# Nipashe

Jumanne Januari 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580451

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





Nipashe

TESA

Jumanne Januari 5, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Corona ilivyomaliza kiuchumi wanawake wawekezaji utalii

NA MWANDISHI WETU

Wenye ualbino wakizingatia haya, watazilinda ngozi zao

UKURASA 11

**Kibano** kwa mabasi yasiyo na tiketi kielektroniki rasmi

UKURASA 3

**Mfanyabiashara** asakwa tuhuma za kutorosha mwanafunzi

UKURASA 4



# JKCI yafanikisha kusimamisha moyo saa 8 kwa upasuaji

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WAZIRI MKUU AAGIZA KUKAMATWA MADIWANI KWA TUHUMA ZA RUSHWA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)...

# Maofisa NIDA wadaiwa kuomba mlungula

UKURASA 3



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Abdul-Razaq Badru (kulia), akimkaribisha Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, katika ofisi za HESLB, jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara ya kikazi jana, katika bodi hiyo na kufanya mazungumzo na menejimenti. **PICHA: HESLB**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store




# IGP awatumia salamu trafiki wala rushwa

UK. 2


**MICHEZO** **SIMBA: FC PLATINUM MBONA MAPEMA TU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood (kushoto), akisikiliza kero ya mmoja wa wafanyabiashara wa Soko Kuu la Morogoro ambao walisitisha jana kwa muda kutoa huduma kwa wananchi kutokana na madai mbalimbali ikiwamo utitiri wa tozo zinazotozwa na Manispaa ya Morogoro. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# IGP awatumia salamu askari wala rushwa

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amesema jeshi hilo limeweka mikakati ya kubaini askari wa usalama barabarani wanaojihusisha na kuomba rushwa ikiwa ni njia ya kulimaliza kabisa suala hilo.

IGP Sirro alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam katika kikao cha tathmini ya utendaji kwa askari wa kikosi cha usalama barabarani wa mikoa ya Dar es Salaam, Rufiji na Pwani.

"Hawa wenye magari mara nyingi wamekuwa wakilalamikia kikosi chetu kwenye suala la rushwa. Kwa hiyo tumekubaliana kwamba haya malalamiko dhidi ya kikosi hicho lazima yapungue. Tumeweka mikakati ya kuhakikisha lazima haya makosa yanayotokana na kuomba na kudai rushwa yanapungua," alisema Sirro.

"Moja ya mkakati ni kuendelea kutoa elimu kwa askari wetu na kwa wananchi pia kupitia vikundi vyetu vya ulinzi shirikishi na kwa kutumia vyombo vya habari. Tunataka kila mtu afike mahali aseme suala la rushwa sasa basi," alisisitiza.

Sirro alipiga marufuku pia askari wa usalama barabarani kuwaweka kwa muda mrefu madereva kwa makosa madogo ya barabarani.

"Kumekuwa na baadhi ya askari ambao si waadilifu ambao wanawaweka madereva masaa (saa) mengi (nyingi) kwa kesi za trafiki, nimesema hapana. Mtu anaweza awekwe masaa (saa) mengi (nyingi) labda kama amesababisha ajali na mtu amekufa ambayo inaonekana kuna ugumu, lakini hakuna sababu ya kukaa muda mrefu kwa makosa ya trafiki," alisema Sirro.

Alisema wako baadhi ya askari ambao wamekamatwa kwa kujihusisha na rushwa na wengine wameshachukuliwa hatua za kisheria kwa kufikishwa mahakamani na kufukuzwa kazi.

"Kwa hiyo kuna makatazo ambayo nimeyatoa kuhakikisha kwamba tunawatendea watu haki na kuwaheshimu ndiyo maana tumeweka mkuu mpya wa kikosi cha usalama barabarani na tayari amepewa maelekezo yake kitu gani afanye. Kwa hiyo ni lazima ifike mahali kikosi kibadilike, kiheshimike na Watanzania waone kwamba kikosi kipo," alisema.

### UKUSANYAJI

Kuhusu madai kwamba alisema jeshi hilo limejiwekea malengo ya ukusanyaji kupitia makosa ya usalama barabarani, Sirro alisema hakuna jambo kama hilo isipokuwa makusanyo yanayopatikana ni kulingana na makosa yanayotokea barabarani.

### WANAOBADILI NAMBA MGARI

Kuhusu watu wanaodaiwa kutokana na makosa ya barabarani, Sirro alisema kumekuwa na baadhi ya madereva hususani wanaomiliki magari mengi, kubadili namba zinazodaiwa na kuweka ambazo hazidaiwi kwa lengo la kukwepa kulipa faini baada ya kuandikiwa.

Kutokana na hilo, alionya kuwa yeyote atakayebainika kufanya hivyo atakamatwa na kushtakiwa kwa kosa la kughushi.

"Kuna watu ambao baada ya kuona kuwa wanadaiwa, wanachofanya ni kuficha magari. Wewe unajua unadaiwa Sh. 200,000 unaamua kuficha gari lako. Niwaombe sana, mkono wa serikali ni mrefu, watawafuata popote walipo, watakamatwa na watachukuliwa hatua kali, huwezi ukaficha gari.

"Lakini wengine wenye magari mengi wanachofanya baada ya kuona gari linadaiwa, anabadilisha namba ya gari ambayo haidaiwi anaiweka kwenye ile ambayo inadaiwa na ukiingia kwenye mfumo inakuwa haisomeki.

"Lakini niseme unapofanya namna hiyo tayari unaingia kwenye makosa ya kughushi, niombe kwa Mtanzania yeyote anayetambua hilo, maelekezo niliyoyatoa ni kwamba wakamatwe, washtakiwe kwa kosa la kughushi," alisema.

### AJALI

Kwa upande wa ajali, alisema jeshi hilo limepunguza ajali za barabarani kwa asilimia 34.

Kuhusu makosa ya ugaidi, alisema jeshi hilo halitamvumilia mtu yeyote atakayebainika kujiingiza katika makosa hayo au kwa wazazi kuzembea kuwadhibiti watoto wao katika kujihusisha na vitendo hivyo.

# JKCI yafanikisha kusimamisha moyo saa nane upasuaji

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imetangaza mafanikio makubwa katika utendaji wake kwa kufanya upasuaji wa mgonjwa, huku moyo ukiwa umesimamishwa hadi saa nane.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni hivi karibuni kwamba huo ni ushindi mkubwa wa miaka mitano tangu kuanzishwa. Alisema hatua hiyo imeipaisha Tanzania katika orodha ya nchi tatu barani Afrika kuendesha operesheni ya aina hiyo.

Prof. Janabi alisema katika hatua hiyo ya umahiri, wamekuwa wakiwahudumia wagonjwa katika operesheni hizo za kusimamisha moyo kwa wastani wa wagonjwa wawili hadi wanne kwa kipindi cha siku tano (wiki moja).

"Tunaweza kuweka mashine kwa mtu mwenye moyo ambao unafanya kazi chini ya asilimia 30, ili kumsaidia.

"Tunaweza kufanya wenyewe upasuaji bila wataalamu kutoka nje kwa kupandikiza mishipa ya damu kwa mtu ambaye mishipa ya damu imebana tukaichukua mishipa kutoka kwenye miguu hadi kwenye mkono," alisema.

Pia alisema mageuzi hayo yanahusu kubadilisha mishipa ambayo mtoto amezaliwa nayo inayochanganya damu safi na chafu na kuirudisha sehemu yake.

Alitaja wagonjwa wanaowahudumia, ambao hadi mwishoni mwa mwaka jana walikuwa 6,500, mbali na nchini, wengine wengi walitoka Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na nchi jirani za Afrika Mashariki.

Daktari huyo bingwa alizitaja nchi zingine za Afrika zilizofikia hatua hiyo ni Comoro na Afrika Kusini na alisisitiza utekelezaji wake kitaaluma kwamba ni ngumu, hali iliyowalazimu kujiwekea utaratibu wa kuanza na sala.

"Kusimamisha moyo wa binadamu, halafu umemaliza upasuaji, kisha unaushtua uanze tena kupiga (moyo kudunda) si jambo rahisi.

"Tunaamini na wenzangu hili liko katika uwezo wa aliyetuumba. Kila upasuaji hatuwezi kuanza bila kusali. Kila mtu huwa anasali kwa imani yake na ndipo tunaanza upasuaji na imekuwa desturi yetu kabla hatujaanza kupita wodini, kliniki tunafanya hivyo tunaona inatusaidia sana," alisema Prof. Janabi.

"Kabla ya kufanya upasuaji wa moyo, tunasimamisha moyo kwa saa tano, sita hadi nane kwa kuitoa damu yote nje kisha baada ya upasuaji tunarudisha moyo, baadhi ya upasuaji huwa tunazifanya wakati moyo ukiendelea kupiga," aliongeza.

Mkurugenzi huyo alisema hadi mwaka jana, taasisi ilikuwa ina umahiri wa kufanya upasuaji wa aina mbili, wakiwamo theluthi mbili wanaofanyiwa upasuaji pasipo kufunguliwa kifua.

Kwa mujibu wa Prof. Janabi, wagonjwa 6,500 walifanyikwa upasuaji na kati yao, wagonjwa 2,041 ndio waliofanyiwa upasuaji wa kufungua kifua.

"Mwaka 2020 upasuaji nyingi zilifanyika miezi ya Aprili na Mei wakati kukiwa na janga la corona. Kipindi hicho, ndipo tuliona umuhimu wa taasisi hii kwa sababu kama utakumbuka mipaka ya nchi mbalimbali duniani ilifungwa, hata kama mtu alikuwa na uwezo wa kifedha waliishia JKCI," alisema.

Prof. Janabi pia alieleza tofauti ya huduma zinazotolewa JKCI na kwingineko nje ya nchi ni kwamba zinapatikana kwenye hospitali binafsi ambako kuna gharama kubwa na hakuna fursa za makundi ya msamaha, utaratibu unaopatikana kwenye hospitali za umma.

Akieleza historia kabla ya kuanzishwa taasisi hiyo, alisema wagonjwa kati ya 400 hadi 500 wanaojumuishwa wa maradhi ya moyo ambao walichukua nusu ya idadi yao, wakiambatana na wanaougua figo na saratani walipelekwa kutibiwa nje ya nchi kila mwaka.

Alisema serikali iligharamia fedha za kianzio dola za Marekani 15,000 (sawa na Sh. milioni 34.5) na kati yao walikuwamo wa makundi ya hatari kama watoto waliozaliwa na hawakuwa na uwezo wa kufikisha umri kati ya mwaka mmoja hadi mitano.

Bingwa huyo pia alilitaja kundi la watu wazima wanaofikishwa hospitali wakiwa wana athari za mshtuko wa moyo, kupona kwao kunahitaji huduma ya ndani ya saa mbili na si vinginevyo.

"Ugonjwa wa moyo ni 'silent killer'. Wengi wetu ukienda hospitali utaambiwa una typhoid (homa ya matumbo), pneumonia, vidonda vya tumbo...vidonda vya tumbo na moyo dalili zake hufanana," alisema.

Prof. Janabi alisema JKCI ilianza kwa hatua ya upasuaji mdogo wa kupandikiza betri moja kwenye moyo na ikapiga hatua hadi kufikia mbili na sasa imefikia umahiri wa kuweka mashine kwenye moyo, unaozuia uwezekano wa kifo cha ghafla inapotokea moyo kusimama.

Kwa upande wa vifo, Prof. Janabi alisema asilimia nane ya wagonjwa waliowahudumia ndiyo walifariki.

Mtaalamu huyo alifafanua kuhusu usalama wa watoto kwamba yako magonjwa ambayo endapo mtoto hajafanyiwa upasuaji katika miezi sita ya kwanza ya uhai wake, hataweza kupasuliwa tena.

"Kuna magonjwa ya kuzaliwa nayo ambayo presha kwenye moyo inakuwa juu sana, umri unapokwenda inazidi, mgonjwa wa aina hii huwezi kumgusa. Hawa tunawapata wengi, huchelewa kuja hospitali na sababu za kuchelewa fedha, kutojua haraka ugonjwa," alisema.

Pia alisema katika safu ya wagonjwa wao watu wazima, ni kawaida ya wagonjwa saba, kati ya wagonjwa 10 wanaowaona wanaugua shinikizo la juu la damu, pindi wakishawachunguza na kwa kiasi kikubwa, wamefanikiwa kuwapunguzia au kuwaondolea matatizo yao.

Alisema uwezo wa utendaji wa JKCI umefanikisha kupunguza wagonjwa wa rufani wanaopelekwa nje ya nchi kwa asilimia 95, asilimia tano pekee ndiyo waendao nje.

HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme wakifungua jengo la ofisi za Halmashauri ya Mji wa Mbinga. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Kibano kwa mabasi yasiyo na tiketi za kielektroniki rasmi

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema kuanzia kesho hakuna wasafirishaji wa mabasi yaendayo mikoani watakaoruhusiwa kufanya hivyo bila kutoa tiketi za kielektroniki kama kanuni zinavyoelekeza.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, kuanzia kesho, hakutakuwapo na basi ambalo litabeba abiria iwapo halitakidhi matakwa hayo.

Hata hivyo, Ngewe alisema agizo hilo litaanza kutekelezwa kwa mabasi yanayofanya safari kutoka Dar es Salaam kwenda Tanga, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Tunduma, Rukwa, Morogoro, Kilombero, Ifakara, Malinyi, Muhenge na njia ya Tanga - Arusha.

Pia LATRA iliwaagiza wasafirishaji wote wa abiria kwa mabasi kuzingatia masharti ya leseni za usafirishaji magari ya abiria zilizotangazwa.

"Kanuni ya 4(2)(c) leseni ya kusafirisha abiria itatolewa kwa mwombaji aliyesajiliwa kwenye mfumo wa tiketi za kielektroniki ulioidhinishwa na mamlaka. Kanuni ya 24(b)(d) msafirishaji mwenye leseni ya kusafirisha abiria wa masafa marefu ahakikishe anatoa tiketi za kielektroniki kwa abiria," ilisema taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo iliongeza kuwa maelezo ya utekelezaji wa agizo hilo kwenye njia nyingine yatatolewa hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hatua hiyo ni utekelezaji wa mkakati iliyowekwa na serikali kwa wasafirishaji na abiria kutokana na kukamilika kwa stendi mpya ya mabasi ya Mbezi ambayo ilianza kutumika Novemba 30, mwaka jana.

Aidha, ilieleza kuwa maagizo hayo yametolewa ili kutatua kero iliyokuwa ikiwakabili abiria kwa kipindi kirefu ikiwa ni pamoja na usumbufu wakati wa kukata tiketi, hasusani nyakati za sikukuu sambamba na kuzidishiwa nauli tofauti na ile iliyoidhinishwa na mamlaka husika.

MNADA WA HADHARA

NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BEST GROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuriya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/NO | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | MJ LIQUOR STORE | MICHAEL JACKSON SWAI | TOYOTA TOWNACE T315DDJ | TABATA KIMANGA | 19/1/2021 NA KUENDELEA |
| ii. | IBRAHIM ELIUD ANOSHI | IBRAHIM ELIUD NANOSHI | NYUMBA | VIKAWE BONDENI,KIBAHA | 20/01/2021 NA KUENDELEA |
| iii. | SHUKRAN JOSEPH MHAWI | MOHAMED RAMADHANI MKATA | NYUMBA | MBEZI JUU,NDUMBWI | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| iv. | SALIM HAMIS MUSHI | SALIM HAMIS MUSHI | KIWANJA | MBWENI | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| v. | FATMA HABIBU ABDALA | FATMA HABIBU ABDALA | NYUMBA | PUGU | 20/01/2021 NA KUENDELEA |
| vi. | CASTOR JOHN RAJABU | CASTOR JOHN RAJABU | NYUMBA | MBEZI JUU SAKUDEVA | 22/01/2021 NA KUENDELEA |
| vii. | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | NYUMBA | USTAWI-BUZURUGA | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| viii. | HADIJA ABUBAKAR PHARES | ABUBAKAR MAYENGA KERABA | NYUMBA YENYE HATI | BUZURUGA | 19/01/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papohapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0713077474 /0754497396
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benkii tarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

# Maofisa NIDA watuhumiwa kudai rushwa utoaji namba vitambulisho

**Na Mwandishi Wetu, KARAGWE**

WANANCHI wilayani Karagwe wamewalalamikia baadhi ya maofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuwaomba rushwa ili wawapatie namba kwa haraka.

Malalamiko hayo waliyatoa katika mikutano ya hadhara ya Mbunge wa jimbo hilo, Innocent Bashungwa, aliyoifanya katika kata mbalimbali, ikiwa ni ziara yake ya kwenda kuwashukuru wananchi kwa kumchagua tena pamoja na kusikiliza kero zinazowakabili.

Kwa mujibu wa wananchi hao, maofisa hao wa NIDA wamekuwa wakifanya hivyo wanapokwenda katika kata kwa ajili ya uandikishaji na kuwataka wananchi hao kutoa fedha kwa madai ya kuwapatia namba bila usumbufu.

Mwananchi aliyejitambulisha kwa jina la Byekwaso, kutoka Kata ya Kanoni, ndiye aliyeibua madai hayo akieleza kukithiri kwa vitendo vya rushwa katika uandikishaji huo.

"Sisi huku tumechukua muda mwingi kwenda kusajili, tumemaliza siku tano pale Rwambaizi. Wakati wanaleta namba za NIDA wengi hatukupatikana kwenye orodha. Pia tunapokuwa kwenye usajili, kuna watu wanataka uwape hela, kweli hiyo hela imetuletea nongwa. Kwa hiyo mheshimiwa mbunge hayo mambo ya NIDA yanaonekana kama hewa tu, wanaopata namba ni wale wenye nacho sisi ambao hatuna hicho hatukupata hizo namba," alisema.

Suala hilo pia lilibuka katika mkutano uliofanyika kata nyingine ambapo wananchi walisema upatikanaji wa namba za NIDA umekuwa mgumu kutokana na kuchukua muda mrefu hatua ambayo imesababisha kufungiwa kwa laini zao za simu, hivyo kukosa mawasiliano na ndugu zao.

Malalamiko hayo pia yaliibulikwa juzi kwenye mkutano uliofanyika kata ya Ihembe, hivyo kumlazimu Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kumpigia simu Mkurugenzi Mkuu wa NIDA huku wananchi wakimsikiliza.

"Mkurugenzi nipo kwenye mkutano katika Kata ya Ihembe, jana nilikuwa na mkutano kata Igurwa na Kanoni lakini kila mkutano wananchi wanapongeza juhudi za serikali kwenye kutatua changamoto, lakini kwenye NIDA mmekuwa majipu.

"Cha kwanza wananchi wanalalamikia mwenye hela ndiye anayepata namba ya NIDA, cha pili hata ambao wamethibitishwa bado wanazungushwa kwa hiyo mkurugenzi nakuagiza kwa upande wa Karagwe fuatilia maofisa wako hawatoshi, hatuna imani nao huku," alisema.

MNADA WA HADHARA

NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BEST GROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuriya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/NO | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | MJ LIQUOR STORE | MICHAEL JACKSON SWAI | TOYOTA TOWNACE T315DDJ | TABATA KIMANGA | 19/1/2021 NA KUENDELEA |
| ii. | IBRAHIM ELIUD ANOSHI | IBRAHIM ELIUD NANOSHI | NYUMBA | VIKAWE BONDENI,KIBAHA | 20/01/2021 NA KUENDELEA |
| iii. | SHUKRAN JOSEPH MHAWI | MOHAMED RAMADHANI MKATA | NYUMBA | MBEZI JUU,NDUMBWI | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| iv. | SALIM HAMIS MUSHI | SALIM HAMIS MUSHI | KIWANJA | MBWENI | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| v. | FATMA HABIBU ABDALA | FATMA HABIBU ABDALA | NYUMBA | PUGU | 20/01/2021 NA KUENDELEA |
| vi. | CASTOR JOHN RAJABU | CASTOR JOHN RAJABU | NYUMBA | MBEZI JUU SAKUDEVA | 22/01/2021 NA KUENDELEA |
| vii. | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | HASSAN BUGANGA KAPOJONGO | NYUMBA | USTAWI-BUZURUGA | 19/01/2021 NA KUENDELEA |
| viii. | HADIJA ABUBAKAR PHARES | ABUBAKAR MAYENGA KERABA | NYUMBA YENYE HATI | BUZURUGA | 19/01/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papohapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0713077474 /0754497396
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benkii tarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

HABARI KITAIFA

# M'biashara asakwa akidaiwa kutorosha mwanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MFANYABIASHARA maarufu mjini Kyela mkoani Mbeya (jina limehifadhiwa), anasakwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kumtorosha mwanafunzi wa kike wa shule ya sekondari (jina la shule linahifadhiwa).

Mfanyabiashara huyo amefunguliwa jalada namba KY4IR/07/2021 katika Kituo cha Polisi Kyela Mjini na kwamba hadi jana Jeshi la Polisi lilikuwa katika harakati za kumsaka eneo la Matema anakodaiwa kujichimbia na binti huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu alisema wanaendelea kulifuatilia suala hilo karibu hadi mtuhumiwa huyo akamatwe. Naye Mkuu wa Wilaya ya Kyela ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta, alipoulizwa kama analifahamu suala hilo alisema: "Nipo jijini Mbeya kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa".

Kwa mujibu wa Matei, Jeshi la Polisi limeshatuma kikosi kazi kwenda Matema Beach kumsaka mfanyabiashara huyo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mtuhumiwa huyo alimtumia ujumbe baba wa binti huyo ukieleza kwamba asihangaike kumtafuta binti yake kwa kuwa alikuwa naye na anataka amuoe.

Akizungumza na Nipashe, baba mzazi wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa) alisema mtoto wake anayesoma kidato cha pili, alitoroshwa na mfanyabiashara huyo Desemba 29, mwaka jana, majira ya saa 1:30 usiku na kumpeleka kwenye moja ya hoteli za kitalii.

Mzazi huyo alisema ilipofika Desemba 30, mwaka jana, mfanyabiashara huyo alimtuma rafiki yake wa karibu kwenda kuonana na wazazi wa mwanafunzi huyo.

"Rafiki wa mfanyabiashara huyo alipokuja kwangu kuniona alinieleza kuwa ametumwa na mfanyabiashara huyo na kwamba tusimtafute mtoto kwani yuko naye na kwamba anaomba amuoe na yuko tayari kutoa hela nitakayohitaji," alisema.

Alisema walikataa ombi la mfanyabiashara huyo kutaka amuoe mtoto wao kinyume cha sheria za nchi, badala yake walimweleza aliyemtuma akamwambie kuwa amrejeshe nyumbani.

Pia alisema walimweleza mshenga huyo kwamba pindi mtoto wao atakaporudi watampima hospitalini kuona kama yuko salama na kwamba endapo atakuwa salama hawatahitaji kuendelea na kesi.

Hata hivyo, tangu Desemba 31, mwaka jana hadi jana mfanyabiashara huyo alikuwa hajamrejesha mwanafunzi huyo nyumbani kwao hatua ambayo ilimfanya baba mzazi kwenda kituo cha polisi Kyela mjini kutoa taarifa.

"Muda huu (saa 4:30 asubuhi) unavyoongea na mimi nipo kituoni hapa polisi nimekuja tangu saa 2:00 asubuhi, lakini nimeambiwa viongozi wa polisi wako kwenye kikao wakimaliza ndipo nitawaona," alisema mzazi huyo.

Nipashe ilipomtafuta mfanyabiashara huyo, alisema yuko tayari kutoa ushirikiano na kwa kuwa suala hilo limesharipotiwa kwenye vyombo husika licha ya kwamba ana nia ya kumuoa.



Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Katibu Kiongozi mstaafu, Dk. Yahya Mzee, akimkabidhi vitendea kazi Katibu Mkuu mpya, Mhandisi Zena Ahmed Said, Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Uchunguzi ajali ya treni waanza

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

ZIKIWA zimepita siku tatu tangu kutokea ajali ya treni eneo la Kigwe wilayani Bahi mkoani Dodoma na kusababisha vifo vya watu watatu, uchunguzi wa kubaini chanzo cha ajali hiyo umeanza.

Kadhalika, majeruhi 63 wa ajali hiyo wameruhusiwa huku watatu wakiwa wamesalia katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, wakiendelea kupatiwa matibabu.

Treni hiyo ya abiria ilikuwa ikitoka Dar es Salaam kwenda Tabora, Mpanda na Mwanza na kupinduka katika eneo la Kigwe.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kazi ya kuondoa mabehewa yaliyodondoka, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema wameanza uchunguzi ili kubaini chanzo cha ajali hiyo.

Kadogosa alisema kuwa uchunguzi huo unafanyika si tu kwa ajili ya kubaini nani amehusika bali pia kusaidia ajali kama hiyo isitokee tena wakati mwingine.

"Lazima tufanye uchunguzi kuangalia kama kweli kuna watu walifanya uhakiki kukagua njia ya treni kabla haijapita, kwa sababu kutoka eneo moja kwenda lingine lazima ufanyike ukaguzi kabla, sasa tutaona kama walipita na kabla hawajarudi maji yalijaa katika eneo lile au ulikuweje," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Stanley Mahundo, alisema juzi walipokea majeruhi 66 wa ajali hiyo.

Muuguzi huyo alisema kati ya majeruhi hao, 32 walilazwa na sita kati yao walifanyiwa upasuaji mkubwa na wengine 34 walipatiwa matibabu na kupewa hifadhi hospitalini hapo wakati wakisubiri usafiri wa kwenda nyuumbani kwao.

Pia alisema majeruhi wote 20 ambao walipekekwa Hospitali ya Wilaya ya Bahi, wameruhusiwa kutokana na afya zao kuimarika. Alifafanua kuwa mpaka sasa wagonjwa waliobaki wodini ni watatu na wanaendelea vizuri.

# Waziri Mkuu aagiza kukamatwa madiwani tuhuma za rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, kuwakamata madiwani na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga wanaokabiliwa na tuhuma za rushwa.

Madiwani hao na kata wanazotoka ni Bruno Kapinga (Mkumbi), Bosco Ndimbo (Lukalasi) na mmoja aliyetajwa kwa jina la Haule (Linda), wakidaiwa kuchukua fedha kutoka kwa watendaji wa Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS), ili kuwashawishi kuhamisha eneo la ujenzi wa makao makuu ya halmashauri hiyo.

Waziri Mkuu, Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizindua jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Mbinga, wilayani Mbinga Mkoa wa Ruvuma.

Pia Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mndeme, kusimamia ujenzi wa halmashauri hiyo, ambao unaendelea katika eneo la Kigonsera.

Agizo la Waziri Mkuu Majaliwa limekuja kutokana na mvutano miongoni mwa madiwani wa halmashauri, huku baadhi kutotaka makao makuu ya halmashauri hiyo kujengwa Kigonsera.

Kutokana na hilo, baadhi yao waliamua kuendesha mchakato wa kushawishi wengine kugomea mradi huo, kukwamisha maendeleo.

Taarifa hiyo ilisema mvutano huo unaongozwa na madiwani wa Kata za Mkumbi, Lukalasi na Linda wakitaka makao makuu kujengwa kwenye kata ya Mkumbi eneo ambalo litaifanya serikali kulipa fidia.

"Hatuwezi kukubali huko mnakotaka nyie ni lazima tulipe fidia ya zaidi ya Sh. milioni 400 na kuna eneo la bure ekari zaidi ya 150.

Hii haikubaliki hatuwezi kufanya mambo ya siasa kwenye fedha za wananchi haiwezekani. Mmeamua kila AMCOS ichange shilingi 600,000 mpate milioni tatu, mfanye kampeni ya kutaka halmashauri ijengwe kwenu, hiyo ni rushwa," alisema.

"Kwa kuwa zile ni fedha za wakulima, Kamanda wa TAKUKURU kawakamate watendaji wa Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS), wahojiwe, kwa nini walitumia fedha kuwapa madiwani wakahonge.

"Waeleze ni nani aliyetoa maagizo ya kutoa shilingi milioni tatu. Hatuwezi kutumia fedha za wananchi kwa ajili ya kuhonga watu, lazima fedha hizo za wakulima zirudishwe ni mali ya wakulima," aliongeza.

Awali, Waziri Mkuu alizindua jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Mbinga na kukagua ujenzi wa nyumba nane za watumishi.

Waziri Mkuu alisema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo, iliyogharimu takribani shilingi bilioni nne na kumpongeza mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Grace Quintine kwa usimamizi mzuri wa miradi huo.

"Tulimletea Sh. milioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba saba za watumishi na ametumia Sh. milioni 321. Pia tulimletea Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mkurugenzi, lakini ametumia Sh. milioni 251 na hakuna ubabaishaji.

Majengo yote yamejengwa kwa viwango bora, endelea kujenga miradi mingine ikiwamo ya vyumba vya madarasa," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Quintine, alisema halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilipekea Sh. milioni 650 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi, zikiwamo za wakuu wa idara na mkurugenzi.

# TANGAZO

## DON BOSCO TECHNICAL TRAINING COLLEGE (DBTTC)

## EMPLOYMENT OPPORTUNITIES

The Salesian of Don Bosco society is one of the largest orders of the Catholic Church that provides education and human development programs for poor, disadvantaged and abandoned children and youths across the world. The Society was founded in 1859 and now includes over 20,000 priests and brothers (Society of St. John Bosco, SDB) and 17,000 sisters (Daughters of Mary Help of Christians, FMA). In furthering their vision and reaching out to more young people in need, they are assisted by thousands of lay supporters and employees in over 136 countries. To date, Salesians run more than 3,500 Salesians schools that include formal and non-formal secondary schools, vocational-technical schools, and agriculture schools, orphanages, and youth centers. The Salesian of Don Bosco society has established with the vision of becoming a center for excellence in innovation and provision of holistic technical education and training. In order to fulfill its functions properly, the College is seeking to recruit qualified and experienced Tanzanians to fill in the following vacancies.

### PRINCIPAL

This is a full time position based in Dodoma, Tanzania. The Principal will serve as the educational leader, responsible for managing policies, regulations, and procedures to ensure that all students are supervised in a safe learning environment that meets the approved curricula and mission of the Institute. Achieving academic excellence requires that the Principal work collaboratively and communicates effectively with the Board of Directors and other stakeholders to direct and nurture all members' staff. The Principal will also be responsibilities for scheduling, curriculum enhancement, extracurricular activities, personnel management, emergency procedures, and facility operations.

**Qualifications and experience required**

- o Holder of a PhD/ Masters in Engineering or Science
- o At least 8 years working experience, three (3) years at a senior position in a related position in any institute of higher learning or management of a technical Institute.
- o He/she must be registered by a relevant professional body.
- o Evidence of training with leadership focus.
- o Evidence of entrepreneurial skills required in managing a technical institution.
- o Management or pedagogical training is an added advantage.
- o He/she must be computer literate.

**Job functions and responsibilities;** The Principal shall:

- Facilitate the transitioning of the current Institute to become the leading technical institution in all spheres.
- Promote and facilitate the innovation and enhancement of the curriculum to ensure it delivers an outstanding range of education and training opportunities.
- Provide support and be responsible for the recruitment of school personnel and faculty to run the maiden programs at the college with a view to grow into a higher learning institution once it starts operating.
- Establish and promote high standards and expectations for all students by ensuring the faculty offers education that is practical/applied, problem-based, and student-centered.
- Organize for attachment of students by ensuring strong alignment with the industry to provide incubation, mentorship, experiential training.
- Manage, evaluate and supervise effective and clear procedures for the operation and functioning of the Institute consistent with its mission, values, and agenda.
- Maintain a positive, cooperative and mutually supportive relationship with staff, parents while communicating with the Board regularly about the needs, successes and general operation of the Institution.
- Be aware and understand relevant legislation and changes in the education sector and the potential implications for the Institution.
- Undertake any additional duties that may be required within the scope of the post.

**Leadership**

- Provide inspiring leadership ensuring that all staff are working in collaboration to achieve the highest results for learners.
- Ensure that the appropriate targets are set and agreed in order to achieve agreed short-term plans and that performance against these targets is monitored and that the college meets these targets.
- Foster positive internal and external communication ensuring staff is made aware of developments and decisions of the management board.
- Be an outstanding ambassador for the Institution promoting and representing it at local, regional and international level.
- Ensure that overall management, internal organization and discipline of staff and learners are consistent with agreed policies and that they are applied fairly.

**Teaching and Learning**

- Ensure that high quality standards are set and achieved for all programmes.
- Promote practices that support learners.
- Supervise the instructional programmes of the school, to encourage the use of a variety of instructional strategies and materials consistent with the college on learning and students growth and development
- Ensure procedures for evaluation and selection of instructional materials and equipment, are according to approved standards
- Ensure evaluation of staff and quality of education, training and services and respond to student's feedback.

**Financial and Resource Management**

- Be responsible to the management board for the preparation of annual estimates of income and expenditure and the efficient, effective management of resources in line with approved budgets.
- Ensure there is proper and effective operation of financial planning and management controls.
- Ensure continued solvency and good financial health of the Institution.
- Ensure that information systems are in place to provide timely robust data to support the management of the Institution.
- Ensure the assets of the Institution are maintained in proper order to avoid deterioration in value and promote further development to support the Institution's objectives.
- Ensure proper repair, stocking of workshops and the library and maintenance of all the college's resources and facilities for promotion of teaching and learning.

### VICE PRINCIPAL ACADEMICS, RESEARCH AND CONSULTANCY

**Qualification:**

Holder of MSc Degree in Engineering/Science. Management and pedagogical training is an added advantage. He/she must have at least three years working experience in a senior management position. He/she must be computer literate.

**Experience:**

Teaching experience in Technical Education institutions for not less than eight years of which three years should be in senior academic position.

Main Duties and Responsibilities:

a) Assists the Principal in all academic matters of the College.
b) Acts as the Principal of the College where by any reason the Principal is unable to act.
c) Ensures smooth operations and development of academics in the College.
d) Advises the Principal on all matters pertaining to academics, research and consultancy.
e) Establishes and maintains a workable system for regular monitoring and evaluation of the performance, quality, relevance and efficiency of all academic programmes.
f) Plans, directs, organizes, monitors and controls all matters related to industrial training of students.
g) Plans, directs, organize, monitors and advice on the recruitment, deployment and development of academic / teaching staff.
h) Reviews existing and develops new academic programmes based on established needs and market signals.
i) Responsible for promoting, planning, implementing, monitoring and controlling research, consultancy and professional activities in the College.
j) Responsible for planning, promoting and advising the Principal on admissions, examinations and student policies and procedures.
k) Develops and maintains academic links with local and International Institutions.
l) Performs any other duties as may be assigned by the Principal from time to time.
m) Evaluating lesson plans and observing classes (teaching, as duties allow) on a regular basis

### VICE PRINCIPAL PLANNING, FINANCEAND ADMINISTRATION

**Qualification:**

Holder of at least a Master's Degree in Engineering/Science, Business Management and pedagogical training is an added advantage. He/she must have at least three years working experience in a senior management position. He/she must be computer literate.

**Experience:**

Experience of not less than eight years in a senior managerial position in the public or private sector

**Main Duties and Responsibilities:**

a) Assists the Principal in all administration and financial matters of the College.
b) Acts as the Principal of the College where by any reason both the Principal and the Vice Principal Academic are unable to act
c) Assists the Principal in all finance and administration matters of the College.
d) Advises the Principal in all matters pertaining to finance and administration.
e) Establishes and maintains workable systems for regular monitoring and evaluation of the performance, quality, relevance and efficiency of all finance and administration programmes.
f) Plans, directs, and organizes, monitors and advices on the recruitment, deployment and development of all staff.
g) Reviews existing and develops new physical, financial, accounting, personnel and administrative programmes based on established needs of the College.
h) Plans and controls all the financial and accounting operations for the College
i) Responsible for the preparation of all financial and accounting reports for the College.
j) Ensures adherence to the approved financial and administrative policies and procedures.
k) Supervises and reprimands staff in accordance with rules and regulations
l) Co-ordinates preparation of budget of the College.
m) Develops training schemes for the College staff.
n) Performs any other duties as may be assigned by the director from time to time.

### REGISTRAR

**Qualifications:**

Possession of a Bachelor Degree in Engineering, Science, Management, education or equivalent from a reputable institution. He/She must have at least five years of relevant working experience at a senior level. He/She must be computer literate.

**Main Duties and Responsibilities:**

a) Heads the Registrar's office of the College.
b) Plans, co-ordinates, direct and controls student admission, examination and related matters of the College.
c) Ensures that the College's adheres to NACTE Examination policies, rules and procedures
d) Ensures that the College's admission, examinations and students registrations and records policy, rules and procedures are followed.
e) Ensures that all correspondences regarding examination results, minutes, rules and regulations are carried out effectively.
f) Ensures efficient consultation with course leaders and sees to smooth scheduling of the assignments in accordance with the Colleges and Governing Board regulation.
g) Arranges the preparation and moderation of draft examination papers in accordance with the Colleges regulations.
h) Ensure examination papers and materials are handled with utmost security.
i) Collects marks from departmental examination officers and compiles for official approval and communication as per the rules & regulations of the College.
j) Performs any duties as may be assigned to him/her from time to time by his/her seniors.

### DEAN OF STUDENTS

**Qualifications:**

Bachelor Degree in Education, Educational Psychology, Counselling and Guidance, Social Work or its equivalent PLUS relevant working experience of not less than six years in a similar institution.

Main Duties and Responsibilities

a) To be an overall in charge of students' welfare at the College
b) To act as principal assistant to the Deputy Principal PFA in all matters pertaining to students' life at the College
c) Secretariat to Students Affairs Committee
d) To handle students' individual problems and provide counselling
e) To undertake the administration of students' welfare services in the areas of accommodation; catering, health and recreation
f) To act as advisor of the students' organization on campus;
g) To supervise the general elections of the student's organizations
h) To co-ordinate the counselling services of the Wardens
i) To perform any other duties as assigned by one's reporting officer.

### TUTOR/INSTRUCTOR I

**Qualifications**

Holder of Bachelor's degree in Mechatronics, Mechanical Engineering or Industrial Automation or Civil Engineering or Hospitality and Hotels or Agriculture or Education with minimum GPA of 3.5 and above or equivalent qualification from recognized Institution.

**Main Duties and Responsibilities**

a) Teaches up to NTA level 6 and may assist teaching in higher NTA levels;
b) Administers examinations for up to NTA level 6 students;
c) Conducts and supports research and consultancy works;
d) Prepares learning resources;
e) Supervises field training;
f) Supervises and assists junior staff; and
g) Performs any other duties as assigned by supervisors.

### TUTOR/INSTRUCTOR II

Bachelor Degree in Mechatronics, Mechanical Engineering or Industrial Automation or Civil Engineering or Hospitality and Hotels or Agriculture or Education with minimum GPA of 3.5 and above or equivalent qualification, registered as technical teacher, who has a working experience in teaching, research and consultancy of at least three years in similar position in related or allied

**Main Duties and Responsibilities**

a) Teaches up to NTA level 6 and may assist teaching in higher NTA levels;
b) Conducts examinations up to NTA level 6;
c) Prepares learning resources;
d) Assumes leadership roles; and
e) Performs any other duties as assigned by supervisors.

**Application Process.**

Interested and qualified candidates should submit their applications, which should include the following:

- Letter of Interest (cover letter) with an indication of the applicant's ability in relation to position applied and availability
- CV or Resume with explaining how your background and experience are relevant to the position you are applying for in terms of; qualifications, competencies, knowledge, and skills
- All applicants will also be required to put at least three names and address of referee

Qualified Candidate should submit their profiles detailing their work Experience and their contacts (with daytime telephone contacts) to **info_Dttc@dbtz.org** while copying **executivedirector@dbtz.org** and **dotz@donbosco.or.tz** by the **15th of January 2021. For information contact 0765 000940 Don Bosco TTC**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi IGP kupambana na rushwa uungwe mkono

**MKUU** wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, jana alitoa tathmini ya utendaji kazi wa askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani katika mikoa ya Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Pwani na Rufiji huku akibainisha matatizo mbalimbali katika idara hiyo ikiwamo vitendo vya rushwa.

Bila kuuma maneno, IGP Sirro aliweka bayana kwamba baadhi ya askari wa kikosi hicho, wamekithiri kwa vitendo vya rushwa ambavyo vimelitia doa jeshi hilo katika ya Watanzania.

Sirro katika taarifa yake hiyo alisema wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka kwa watu wenye magari kwamba askari wa kikosi hicho wamekuwa wakiomba na kupokea rushwa, hatua ambayo imekuwa kero kwao na upande mwingine inalitia doa jeshi hilo.

Moja ya njia ambazo askari hao wamekuwa wakitumia kujihalalishia rushwa ni kuwasimamisha kwa muda mrefu madereva na wenye magari kwa makosa madogo madogo bila sababu za msingi.

Kutokana na hali hiyo, alisema jeshi hilo limejipanga kumaliza tatizo hilo na njia mojawapo katika kufikia azma hiyo ni kubaini askari wanaojihusisha na kuomba rushwa na kuwachukulia hatua.

Moja ya mkakati katika kupambana na tatizo hilo, kwa mujibu wa kiongozi huyo mkuu wa polisi, ni mabadiliko ambayo yamefanywa ndani ya kikosi hicho kwa kuteua kamanda mpya. Alisema mkuu huyo wa trafiki, Wilbroad Mutafungwa, ameshapewa maagizo namna ya kulishughulikia tatizo hilo.

Sambamba na hatua hiyo, Sirro alisema wataendelea kutoa elimu kwa askari na wananchi kupitia vikundi vya ulinzi shirikishi na kutumia vyombo vya habari.

Hatua ya IGP Sirro ya kuweka bayana vitendo vinavyofanywa na askari ili kuhalalisha rushwa, inaonyesha dhahiri kwamba amedhamiria kuchukua hatua stahiki baada ya kuwapo malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi, huku baadhi ya maofisa wa ngazi za juu wa jeshi hilo wakiwakingia kifua wahusika.

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba askari hao wanafanya hivyo kwa kutumwa na baadhi ya wakubwa wao wakiwamo maofisa wa usalama barabarani wa mikoa na taarifa zinaopowafikia wanakuwa wakali kwa wananchi.

Ni ukweli kwamba baadhi ya askari wa usalama barabarani wamekuwa vinara katika kulipaka tope Jeshi la Polisi kutokana na kuendekeza rushwa. Baadhi ya askari hao, kama alivyosema IGP, wamekuwa wakijificha kwenye vichaka au sehemu ambazo si rahisi kubainika kuwa wanapokea rushwa.


Katika barabara za mikoani kama kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro na Tanga, kuna maeneo kadhaa ambayo wametengeneza vijiwe kwa ajili ya kuwasimamisha madereva kwa madai ya kukagua au kudai kwamba wamezidisha mwendo. Lengo kubwa la kufanya hivyo ni kutaka rushwa.

Kama alivyosema IGP vitendo vya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi vinapaswa kufika mwisho. Njia muhimu katika kufikia hilo ni maofisa wa juu wa polisi kutoa namba zao ili wananchi wanaoathirika na vitendo hivyo watoe taarifa kwao. Polisi bila rushwa inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# TCRA waonye waunganisha miito simu kinyemela, kijanja

Na Mwandishi Wetu

**WIKI** iliyopita Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa miezi mitatu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kutatua tatizo la vifurushi na bando kwenye simu na jinsi linavyoyeyuka kwa kasi, wateja wakihoji kulikoni?

Alipotembelea TCRA alisema mamlaka hiyo ishughulikie tatizo hilo ili kampuni za simu zitatue tatizo la bando na vifurushi. Matumizi ya simu kwa dunia ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hayaepukiki kutokana na mapinduzi ya kiteknolojia katika sekta zote bila kujali ni mjini au kijijini, au maskini au tajiri.

Takwimu zinaonyesha kuwa watumiaji wa intaneti wameongezeka duniani na kufikia watu bilioni 4.5 na kati yao watumiaji milioni 23 wanatoka Tanzania. Simu za mkononi zimekuwa tegemeo kubwa kokote duniani zikiwamo nchi zinazoendelea ambako uchumi wa wananchi wake hauzidi Dola mbili kwa siku (Shilingi 5,000).

Ili kuhakikisha mtu anayemiliki simu kwa siku anaitumia kwa tija, inamlazimu kutenga angalau kiasi cha Sh. 500, hadi 1,000 kwa matumzi ya mawasiliano mbalimbali, lakini hasa kifurushi cha intaneti ili kumwezesha kuperuzi taarifa mbalimbali mitandaoni.

Pamoja na gharama hizo, baadhi ya watoa huduma hizi wamekuwa wakilalamikiwa kuwa mbali na maelezo ya huduma wanayojiunga kuelezea anachokitaka, kuna mambo mengine wanayopewa nyuma ya pazia bila kushirikishwa ambayo wateja wanayahoji.

Kwa mfano miito ya simu kwamba anayepigiwa simu atausikia muito huo hasa wimbo wa msanii fulani, imekuwa huduma inayounganishwa kwa lazima kwa baadhi ya wateja ambao hulazimika kuzilipia pengine bila ridhaa yao.

> **Waziri Ndugulile aligusia suala hili pengine kutokana kukithiri kwa malalamiko kwenda kwa kampuni za simu za mkononi kutoka kwa wateja akisema, wapo wanaosema wakosa imani na vifurushi vya intaneti.**

Ikumbukwe mteja anaweka vocha yake, ili ajiunge na huduma ya kupiga simu au kifurushi kwa ajili ya kuperuzi taarifa nyingine iwe 'face book, Whatsap, twita na instagram' lakini hata kabla ya kujiunga vocha imemalizika pasipo kujua. Anabakia na malalamiko na uchungu, imekuwaje?

Kuna uwezekano wa baadhi ya mifumo ya kiteknolojia kumuunganisha mteja pasipo ridhaa yake na huduma hiyo, ambayo pengine haihitaji. Ni vyema kampuni zinazohusika kufahamu kuwa hilo halimridhishi mteja wao.

Kinachotokea kwa baadhi ya watoa huduma za simu za mikononi, kuwapigia baadhi ya wateja wao kwa namba ambayo haitambuliki na mteja akipokea huungwa na muito pasipo ridhaa yake. Lakini huduma hiyo ya muito kwa ambao wameunganishwa bila ridhaa, wanaeleza kuwa, hawakujiunga nayo ingawa kila wanapoweka vocha, wanakuta pesa imekatwa kulipia miito.

Waziri Ndugulile aligusia suala hili pengine kutokana kukithiri kwa malalamiko kwenda kwa kampuni za simu za mkononi kutoka kwa wateja akisema, wapo wanaosema wakosa imani na vifurushi vya intaneti.

Ni ukweli kuwa mteja anayenunua muda wa maongezi au vocha amejipima matumizi yake kwa siku, wiki na hata mwezi kulingana na uwezo wake, inapoingia gharama au kuunganishwa huduma pasipo ridhaa anaanza kuona gharama za ziada.

Kutokana hilo mamlaka husika ziliangalie kwa kuwa wanaoathirika na hilo ni ambao wana kipato cha chini wakitegemea kutumia simu kulingana na pesa yao, lakini wanakatishwa tamaa na baadhi ya wajanja ambao wanawaingiza katika mitego kama hiyo.

Katika hili wengi wanaumizwa pasipo kufahamu, lakini waziri ameyaona na kuyasikia malalamiko yao hivyo ni vyema TCRA ikaliona na kulitolea ufumbuzi.

HABARI KITAIFA

# Mchungaji TAG adaiwa kupotea

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Tanzania Asseblies of God (TAG) Kitangili, mjini Shinyanga, Paulo Msangi, amedaiwa kupotea mwezi mmoja sasa na kuiacha familia katika hali ngumu kimaisha.

Beatrice Mdei, ambaye ni mke wa mchungaji huyo, alisema jana kuwa mume wake aliondoka Novemba 30, mwaka jana, akiaga kuwa anakwenda Mpanda kufuata mchele wa biashara, lakini muda mfupi baadaye simu yake haikupatikana tena na hawajui aliko.

Alisema mume wake huyo mbali na uchungaji, alikuwa akifanya biashara ya kuuza mchele na kuusafirisha kwenda kwenye mikoa mbalimbali ikiwamo Arusha na Kilimanjaro, lakini tangu aage kwenda Mpanda, hajapatikana huku wakiendelea kuhangaika kumtafuta.

"Mimi ni mama wa nyumbani na sina kazi yoyote ya kufanya na tuna watoto watatu na wanasoma katika shule za kulipia na wanamtegemea baba yako kwa kila kitu. Sasa hivi tunaishi maisha magumu ya kuomba omba chakula, nasaidiwa na waumini pamoja na kutumiwa chakula kutoka nyumbani kwetu Moshi," alisema Mdei.

"Tumepiga simu kwa rafiki zake nao wanasema hawajui alipo na hawana mawasiliano naye. Wakimpigia simu yake haipatikani, hivyo naomba serikali inisaidie kumpata mume wangu, napata shida ya kulea watoto mwenyewe na mimi sina hata kazi," aliongeza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema taarifa za mchungaji huyo kudaiwa kupotea wamezipata na wanazifanyia kazi.

# Mbaroni kwa madai ya kumpiga mtoto hadi kufa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Amos Ludovick (39) mkazi wa kijiji Ibale wilayani Kyerwa, kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mtoto wake Dastan Amos (13).

Mzazi huyo anadaiwa amesababisha kifo cha mtoto huyo baada ya kumchapa kwa fimbo sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Jumamosi iliyopita baada ya mtoto huyo ambaye alikuwa mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Ibale, kuondoka nyumbani kwao kwenda kutembea bila idhini ya wazazi na kurejea saa 9:00 alasiri.

"Huyu mtoto alipohojiwa na baba yake hakutoa majibu yanayoridhisha ndipo baba alianza kumchapa kwa fimbo sehemu mbalimbali za mwili wake bila kumhurumia. Baada ya kumchapa, mtoto huyo alikwenda kulala chumbani na ilipofika usiku saa 3:00 wakaona mtoto haamki. Walikwenda chumbani na kukuta tayari amefariki (dunia)" alisema.

Kamanda Malimu alisema uchunguzi wa kitabibu uliofanyika ilibaini kuwa mtoto huyo alivunjika shingo na uti wa mgogo na kuwa ndicho chanzo cha kifo chake.

Pia kamanda huyo alisema, jeshi hilo linaendelea kuchunguza tukio la Jesca Samson (37) mkazi wa kijiji Ruzinga wilayani Karagwe, aliyefariki dunia kwa kunywa sumu ya panya ambayo pia alimnywesha mtoto wake Jordan Samson (3) ambaye amenusurika kifo baada ya kukimbizwa hospitali ya Nyakahanga.

"Huyu mama alikuwa na ugomvi wa kifamilia na mume wake baada ya mume kuuza ardhi bila kumshirikisha. Malalamiko hayo yalifika hadi mahakamani na kusababisha baba kukamatwa," alisema.

Alisema baada ya ugomvi huo, mama huyo alihama na kwenda kuishi kwa ndugu zake, Dotto Clemence na Evodia Mussa, na kwamba Desemba 31, waliondoka nyumbani wote watatu kwenda Kayanga mjini kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya.

"Mwaka mpya uliwakuta huko lakini baada ya sherehe, mama huyo aliondoka na ndugu zake kurejea nyumbani, wakiwa njiani aliwatoroka na kukimbia kurudi nyumbani haraka, alipofika akanywa sumu na kumnywesha mtoto wake" alisema.

Alisema baada ya ndugu zake kufika walimkuta hajakata roho wakamchukua yeye na mtoto wake na kuwapeleka hospitali ya Nyakahanga, alikofia wakati akipatiwa matibabu.

Kamanda huyo alisema uamuzi wa mama huyo kujiua ulifanyika siku moja baada ya mume wake kurejea kutoka gerezani alikokaa kwa takriban miezi mitatu kutokana na kesi hiyo ya kuuza ardhi.




Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini, Gilliard Ngewe (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Salum Pazzy - Ofisa Habari Mwandamizi LATRA (kushoto) na Tadei Mwita ambaye ni Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri akunwa kasi ujenzi wa hospitali

**Na Munir Shemweta,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameelezea kuridhishwa na ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mtwara wa ghamara ya Sh. bilioni 16 na kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kazi hiyo nzuri.

Hospitali hiyo itakapokamilika, itahudumia wananchi wa mikoa ya Kusini na nchi jirani, Dk. Mabula alieleza hayo jana alipokuwa katika siku ya kwanza ya ziara yake katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

Alisema pamoja na NHC kuwa na changamoto ya kifedha, iliamua kutumia fedha zake takriban bilioni 2.4, ili kuharakisha ujenzi huo wakati likisubiri malipo yake ya Sh. bilioni 2.7.

Mabula alisema uamuzi wa shirika hilo kutumia fedha zake una lengo la kuhakikisha mradi hausimami na wakati huo huo kuharakisha ujenzi wa mradi huo kukamilika, hivyo kuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma pamoja na nchi jirani.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, hospitali hiyo pamoja na kutumika kwa huduma za kitabibu na mafunzo, eneo la hospitali hiyo linaweza kutumika kama sehemu ya utalii kutokana na kujengwa katika eneo la ufukweni mwa Bahari ya Hindi.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri aliitaka idara ya ardhi katika Halmashauri ya Mtwara/Mikindani kuhakikisha eneo hilo linapangwa katika sura ya kitalii.

"Eneo hili ilipojengwa hospitali ni zuri na linaweza kutumika pia katika utalii. Naiagiza idara ya ardhi kuweka mpango wa eneo hili utakaoendana na shughuli za utalii kwani kuna fursa inayoweza kumfanya mgonjwa kupata nafuu," alisema.

Naye Mbunge wa Nanyamba, Dadi Chikota, aliishukuru serikali kwa usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa hospitali hiyo na kuipongeza NHC kwa kasi ya ujenzi na umakini wa hali ya juu unaofanya jengo hilo kuwa na ubora.

Awali, ujenzi wa hospitali hiyo ulitarajiwa kukamilika Septemba, mwaka jana, lakini sasa uko katika hatua nzuri na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

# HABARI PICHA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Sadifa Juma Khamis kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja, katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Ikulu, Zanzibar. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Karagwe na Diwani wa Nyaishozi, Wallace Mashanda, akisisitiza suala la wanafunzi kupatiwa uji na chakula shuleni katika mkutano wa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Karagwe, Innocent Bashungwa, katika Kata ya Nyakasimbi, juzi. **PICHA: ELIUD RWECHUNGURA**




Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya China Railway Seventh Group, wakipanga mawe kwa ajili ya kujenga ukingo wa maji katika eneo la Chang'ombe Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akishuka ngazi wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mtwara wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na miradi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**



Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (wa pili kushoto), akisalimiana na baadhi ya wazee wa Mtaa wa Olkungu, Kata ya Terrat jana, wakati wa mwendelezo wa ziara yake ya kusikiliza kero za wananchii wa jimbo hilo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

HABARI KITAIFA

# W'biashara wagoma kutoa huduma kisa utitiri tozo

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

WAFANYABIASHARA wa soko kuu lililoanza takribani siku mbili, wamesitisha kwa muda kutoa huduma kwa wananchi wakishinikiza uongozi wa Manispaa ya Morogoro kupunguza utitiri wa tozo zinachangia kupata hasara.

Soko hilo lilojengwa upya na kuanza kutumika Januari Mosi, mwaka huu, na wafanyabiashara waliopisha ujenzi na baadaye kurudishwa kuendelea na biashara katika soko hilo, jana walitangaza kusimamisha huduma.

Kwa mujibu wa wafanyabiashara hao, manispaa imeweka tozo mbalimbali ambazo kwa sasa zimekuwa kikwazo kwao katika kufanya biashara kwa faida.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Athumani Salumu, alimweleza Mbunge wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, ambaye alifanya ziara ya gafla kufuatia mgomo huo katika soko hilo kuwa moja ya tozo hizo ni pamoja kuingiza bidhaa kutoka masoko mengine ya jumla.

"Soko hili kuu halina wafanyabiashara wanauza bidhaa za jumla, hivyo tunalazimika kwenda kununua bidhaa kama ndizi katika masoko mengine likiwamo la Mawenzi na tunaleta katika soko kuu.

"Tunatumia usafiri wa pikipiki, lakini wanatoza Sh. 500 kwa kila safari na tunaweza kuleta zaidi ya safari tano mpaka sita wakati katika soko hilo kuna pikipiki zinazoegeshwa kwa siku kila moja inatozwa Sh. 1,000," alisema Salum.

Mfanyabiashara mwingine, Juliana Siogopi, anayeuza nafaka, alisema kuna watu wamehodhi vizimba na kuwapandishia bei kutoka Sh. 20,000 inayolipwa manispaa hadi Sh. 50,000 mpaka 70,000 jambo ambalo limekuwa likiwasababishia mazingira ya biashara yao kuwa magumu.

"Hivi vizimba kule manispaa vinalipiwa Sh. 20,000 na sisi tuliomba na kufuata utaratibu uliwekwa, lakini tukakosa ila kuna watu wamepewa vizimba, lakini si wafanyabiashara, hivyo inabidi tupange kwa Sh. 50,000. Tunaomba tusaidiwe kupatiwa vizimba kwa gharama ya manispaa," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo, Abood alisema amebaini kuna kero na kuahidi kuwakutanisha viongozi wa soko na manispaa kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi.

"Hapa ninaye mkurugenzi wa manispaa, nitamkabidhi kero zenu zote ataenda kuzifanyia kazi baada ya kukutana kwenye kikao cha pamoja akiwamo mwakilishi wenu katika soko hili," alisema Abood.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheila Lukuba, alikiri kuwapo kwa kero za wafanyabiashara hao kutokana na soko hilo kuwa ni jipya na linachukua watu wengi na kero hizo zitatuliwa moja baada ya nyingine.

Alisema kutokana na soko hilo kuwa jipya, kuna maelezo yametolewa na wafanyabiashara ya kupandishiwa gharama za vizimba hivyo kuahidi kulitafutia suala hilo ufunbuzi ndani ya miezi miwili.

Soko Kuu la Morogoro lenye fremu kadhaa za maduka na vizimba 900, lilijengwa kisasa kwa ghorofa moja baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kuipatia Manispaa ya Morogoro Sh. bilioni 17.6 baada ya soko la zamani lililojengwa mwaka 1953 kuvunjwa.



Diwani wa Kata ya Chumbageni jijini Tanga, Ernest Kimaya (kulia), akitoa maelezo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Chumbageni kwa Mbunge wa Jimbo la Tanga ambaye ni Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu, jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Barabara ya Rukwa kujengwa kwa lami

Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, amesema serikali iko mbioni kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kilyamatundu hadi Usevya, iliyoko katika bonde la Ziwa Rukwa ili kuondokana na changamoto ya kuikarabati mara kwa mara, hivyo kugharimu fedha nyingi.

Alisema hayo jana alipokuwa akikagua miundombinu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 200, ambayo baadhi ya madaraja yake yalisombwa na maji kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha wilayani hapa.

Kasekenya alisema kila mwaka serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara hiyo, hususani madaraja, hivyo suluhisho la kudumu ni kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

"Kwa muda huu mfupi tunapambana kuhakikisha miundombinu yote iliyoharibika inarejeshwa katika hali yake ili barabara ipitika muda wote. Kwa suluhisho la kudumu tutaijenga kwa lami na bahati nzuri msanifu wa mradi anaendelea na kazi pindi michoro itakapokamilika, tutaanza ujenzi," alisema.

Naye Mbunge wa Kwela, Deus Sangu, alisema tathmini iliyofanywa na wataalamu wa ujenzi kutoka Wakala wa Barabara (TANROADS) ni kwamba madaraja manane yamesombwa na maji ya mvua na matengenezo yake yatagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.4.

Sangu aliishukuru serikali kwa kuchukua hatua za haraka kufanya marekebisho ya barabara hiyo kwa kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi ya mkoa wa Rukwa, ikizingatiwa kuwa bonde hilo linategemewa kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hususani mpunga.

"Hili ni eneo la kiuzalishaji na wafanyabiashia wengi wapo huku kununua mazao hususani mahindi na mpunga. Sasa inapojitokeza hali ya kukatika kwa mawasiliano wanaathirika sana namna ya kupeleka bidhaa zao sokoni. Kwa hiyo hatua kama hizi za haraka zinatia faraja," alisisitiza Sangu.

**"Kwa muda huu mfupi tunapambana kuhakikisha miundombinu yote iliyoharibika inarejeshwa katika hali yake ili barabara ipitika muda wote. Kwa suluhisho la kudumu tutaijenga kwa lami na bahati nzuri msanifu wa mradi anaendelea na kazi pindi michoro itakapokamilika, tutaanza ujenzi," alisema.**

# DC akemea wanaoendekeza makundi

Na Mohab Dominick, BUKOMBE

MKUU wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wanasiasa wilayani hapa, kutoendekeza makundi jambo ambalo litawafanya kutotekeleza vyema ilani ya uchaguzi.

Nkumba amewataka wanachama na wanasiasa hao wawe na makundi yenye tija ili kuimarisha chama na kuongeza kasi ya maendeleo ya wilaya kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye sherehe ya kuukaribisha mwaka mpya, iliyoandaliwa na Mbunge wa Bukombe, Doto Biteko, na kufanyika nyumbani kwake kijiji cha Bulangwa.

"Niwasii tutumie nafasi na niwaombe tutumie nafasi hii leo (juzi). Maisha yetu haya yana changamoto nyingi, hapa katikati tulikuwa na mambo mengi tulikuwa na uchaguzi na wengine hata ukiisha wao hawamalizi uchaguzi," alisema.

Alisema wako baadhi ya wanachama wanaendeleza midahalo juu ya wagombea waliopita na kwamba pengine hiyo ni kwa sababu aliyepita hawakumtaka.

Pia aliwataka viongozi wa kisiasa na watendaji katika Halmashauri ya Wilaya hiyo kuvunja makundi na kutumia fursa ya mwaka mpya kila mmoja kufungua moyo ili kuondoa dukuduku na badala yake wafanye kazi za maendeleo kwa lengo la kuifanya Bukombe ipige hatua zaidi.

"Kwenye kila kata tuna diwani mmoja mmoja na hata ngazi ya mwenyekiti wa halmashauri tunaye mmoja tu. Hawa wengine wanatoka wapi? Vunjeni makundi na mfanye kazi za maendeleo kwa wananchi," alisema.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa wilaya alisema katika elimu, wilaya ya Bukombe inaongoza kwa ufaulu mzuri katika mkoa mzima wa Geita na kutaja kuwa zaidi ya wanafunzi 5,000 wamefaulu kujiunga na kidato cha kwanza.

Nkumba alitumia mwanya huo kuwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka shuleni watoto hao.

"Kwa sasa Wilaya ya Bukombe inaendelea kushika nafasi ya kwanza katika mitihani ya taifa kwa mkoa wa Geita na tutahakikisha kila mtoto aliyefaulu kujiunga kidato cha kwanza, anakwenda. Tulishafanya uhakiki na kwamba zaidi ya wanafunzi 5,000 waliofaulu wanakwenda kuanza masomo yao," alisema.

Naye Mbunge wa Bukombe na Waziri wa Madini, Doto Biteko, alisema hizo ni juhudi zinazotokana na umoja, mshikamano walio nao viongozi wa wilaya na ndiyo sababu kubwa iliyowafanya waongoze kimkoa kwa upande wa elimu.

# Wakulima korosho Tunduru wafundwa kuhusu matapeli

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

WAKULIMA wa korosho wilayani Tunduru, wametakiwa kutokuwatumia watu wasiowafahamu kuwasaidia kutoa fedha benki, ili kuepuka vitendo vya kutapeliwa na kuibiwa fedha zao.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Tunduru (TAMCU), Hashim Mbalabala, alipokuwa akizungumza na wakulima waliouza korosho kwenye mnada wa 11 uliofanyika katika viwanja vya Chama cha Msingi (AMCOS) Mlingoti Mashariki.

Mbalabala alisema chama kikuu kinazo taarifa za wakulima kutapelewa na kuibiwa fedha zao na makundi ya vijana ambao wamekuwa wakijifanya wasamalia wema kujitolea kuwasaidia wazee kutoa fedha zao kupitia mitandao ya simu na ATM za benki.

Alisema vijana hao, baada ya kujua namba za siri za simu na ATM, huhamisha fedha kwenda kwenye akaunti au namba zao za simu na kutokomea.

Mwenyekiti huyo alisema ingawa matukio ya wizi yanaonekana kupungua katika mzimu huu wa mwaka 2020/21 ni tofauti na msimu wa mwaka 2019/20, kundi la wazee bado linaandamwa na vijana hao kwa ajili ya kuwaibia fedha zao.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wazee kuacha tabia ya kuhamisha fedha zote kwenye akaunti zao na wakati wanapokwenda kuchukua wawatumie ndugu au vijana wao.

Katika mnada huo ambao walijitokeza wanunuzi watano na kati yao mnunuzi mmoja ambaye aliomba kununua korosho zote kupitia maombi ya barua, wakulima hao waliuza koshoro zote kwa Sh. 2,100 kwa kilo daraja la kwanza daraja la pili kwa Sh. 1,622.

Awali, Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, alisema kilo 183,328 za daraja la kwanza na kilo 55,659 daraja la pili, ziliwekwa mtandaoni kwa ajili ya kuwataka wanunuzi kushindania kuzinunua kupitia utaratibu wa kuomba kuzinunua kupitia barua za kutumbukiza kwenye sanduku na mfumo wa mtandao TMX.

Bisani alisema kutokana na mauzo hayo, Sh. 475,367,698 zilipatikana na zinatarajiwa kuingizwa kwenya akaunti za wakulima baada ya taratabu za malipo kutoka kwa mnunuzi aliyeshinda kukamilika.

Meneja Mkuu wa TAMCU, Imani Kalembo, alisema mwenendo wa malipo unakwenda vizuri na kwamba hadi sasa ofisi yake imekwishaidhinisha malipo ya minada 10 kwa vyama vya msingi kwa ajili ya kuwalipa wakulima wao.



Meneja wa Benki ya Azania tawi la Kagongwa, Prosper Meela (mwenye suti), akikabidhi funguo kwa mwenyekiti wa waendesha bodaboda Kagongwa, Samweli Malale (aliyevaa kofia ngumu), kwa niaba ya wenzake tisa ambao wamepewa mkopo na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ndikilo ataka wabadhirifu wadhibitiwe

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameziagiza halmashauri za mkoa wa Pwani, kuwafuatilia watendaji wanaotuhumiwa kujinufaisha kupitia mapato ili wadhibitiwe mapema.

Ndikilo alisema jana kuwa kila halmashauri inatakiwa kuwafahamu watendaji wanaohusika kuvujisha mapato ili wadhibitiwe na kutafuta namna ya kukomesha tabia hiyo.

Pia alizitaka halmashauri kujikita kukisanya mapato, ili kukidhi kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema mabaraza ya madiwani yanatakiwa kukaa na watendaji kupitia upya mikataba iliyotiwa saini na halmashauri kama kuna kipengele cha kuhujumu kiondolewe.

Ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri, alisema unasaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo imepangwa badala ya kusubiri fedha kutoka Serikali Kuu.

Aidha, aliwaelekeza wakurugenzi wanapoanza kutoa vitambulisho vya wajasiriamali kuanzia mwezi huu kila anayehitaji aonyeshe alichokuwa akitumia awali.

Ndikilo alitoa maagizo hayo baada ya taarifa iliyoeleza kuwa kati ya vitambulisho vya wajasiriamali 65,500 vilivyotolewa ni 14,000 pekee vilivyochukuliwa.

Alisema kasi ya wajasiriamali kuchukua vitambulisho hivyo bado ni ndogo, hivyo kila mkurugenzi anatakiwa kuhakikisha anatilia mkazo suala hilo.

**Alisema mabaraza ya madiwani yanatakiwa kukaa na watendaji kupitia upya mikataba iliyotiwa saini na halmashauri kama kuna kipengele cha kuhujumu kiondolewe.**

# Wanafunzi wote kujiunga na sekondari

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

WANAFUNZI 154 waliomaliza elimu ya msingi mwaka jana katika Kata ya Nyamilangano Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, watajiunga na kidato cha kwanza kutokana na ujenzi wa nyumba vitatu vya madarasa kukamilika kwa wakati.

Wanafunzi hao wataingia kidato cha kwanza katika sekondari ya Kisuke huku wengine wakitoka katika shule zilizoko katika kata jirani za Nyamilangano, Kisuke, Bukomela na Mapamba.

Diwani wa Nyamilangano, Robert Maganga, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii na kuongeza kuwa wanafunzi hao 154 wanatoka katika shule za msingi tisa ambazo zinategemea shule hiyo moja ya sekondari.

Maganga alisema kuwa ujenzi huo wa madarasa matatu kwa sasa uko katika hatua za mwisho na umefanyika kwa ushirikiano baina ya halmashauri na wananchi wa kata hiyo lengo likiwa kuwawezesha wanafunzi waliofaulu kupata nafasi.

Maganga alisema maandalizi mpaka sasa kwa wanafunzi hao yako tayari huku akisisitiza kuwa hadi shule zitakapofunguliwa, madarasa yote yatakuwa yamekamilika na wanafunzi wataingia madarasani kama ilivyopangwa.

"Katika kata yangu hakuna mwanafunzi ambaye amemaliza darasa la saba mwaka jana na kukosa kuingia kidato cha kwanza kwa ukosefu wa vyumba vya madarasa labda iwe sababu nyingine kwani hapa madarasa ndiyo yanayowasubiri wanafunzi waanze masomo kwa wakati," alisema Maganga.

Alisema mbali na kumaliza ujenzi wa vyumba vya madarasa, pia kumekuwa na upungufu wa madawati katika sekondari hiyo.

Kutokana na upungufu huyo, tayari amekwishapata msaada wa madawati 50 kutoka Benki ya NMB Tawi la Kahama ambayo yatasaidia kupunguza tatizo hilo huku wazazi nao wakifanya jitihada za kuona ni jinsi gani madawati yanaweza kupatikana na kuondokana na adha hiyo.

Diwani huyo pia alishukuru ushirikiano ulionyeshwa na Halmashauri ya Ushetu katika kuhakikisha wanafunzi hao wanaingia madarasani kwa kuonyesha nguvu zake kuchangia katika mahitaji mbalimbali yaliokuwayakitakiwa katika shule hiyo ya sekondari iliyoko katika makao makuu ya halmashauri hiyo.

Maganga pia aliwashukuru wananchi kwa kuonyesha kujali kuchangia shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa vyumba hivyo vya madarasa hali ambayo itasaidia wanafunzi kuingia madarasani kwa wakati.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 5, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 12

## Corona ilivyomaliza kiuchumi wanawake wawekezaji utalii



Ukurasa 14

**Wazoefu maisha vijiweni walipogeuka wakulima stadi**



Ukurasa 13

Gitanjali Rao mwanasayansi kinda aliyetikisa dunia 2020

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Wenye ualbino wakizingatia haya, watazilinda ngozi zao

JUA kali linalowaka karibu kila mahali, wataalamu wanalielezea kuwa ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi yanayochochea ongezeko la joto duniani, lakini pamoja na maradhi kwa watu na mimea.

Wanaonya kuwa jua hilo lina mionzi mikali ambayo haiwaachi watu salama likiumiza zaidi ngozi na macho.

Miongoni mwa wanaoathirika zaidi ni wenye ualbino ambao wanakosa au kupungukiwa na rangi ya asili kwenye macho na ngozi. Ngozi yao inaathiriwa na mionzi mikali ya jua Ultra Violet (UV).

Kutokana na jua na mabadiliko ya hali ya hewa wanashauriwa kuchukua tahadhari kwanza wapunguze, au kuacha kutembea wakati wa jua kali kama siyo lazima na ikibidi wasifanye kazi wakati huo.

Aidha, wanakumbushwa kuvaa mavazi ya pamba wala si nailoni au mpira, yanayowafunika mikono, kofia kuziua jua usoni, mchoni na kichwani. Miguu nayo ifunikwe na pia ni vyema kuvaa miwani kuzuia jua lisiumize kiio (lenzi) ya jicho.

Kwa sasa mabadiliko ya tabianchi yameleta jua kali pamoja na kuongeza joto, vipi watu wenye ualbino wanahamasishwa kujilindaje na athari za jua kali? Vipi kuhusu kupatiwa mafuta kinga ya kulinda ngozi na mionzi hatarishi ya jua inayoleta saratani?

Ni swali Nipashe inayomuuliza Mfamasia Mkuu wa Serikali Daudi Msasi, anayejibu kwa kueleza kuwa serikali inalijua tatizo hilo na inatoa bure mafuta ya kulinda na kukinga ngozi za wenye ualbino dhidi ya mionzi hatarishi.



Watoto wakiwa juani wafunikwe kichwa, shingo na miguu wasiachwe viungo vyao viumizwe na mionzi hatarishi ya jua. **PICHA: MTANDAO**

Msasi anasema tangu mwaka jana serikali ilitangaza bungeni kuwa dawa au mafuta hayo ya 'sun screen' yaanze kutolewa bure kwa wanaoishi na ualbino kwamba yanapatikana kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali zote za serikali na hayauzwi.

"Wanatakiwa kupatiwa dawa bure kwenye vituo vya kutolea huduma iwe zahanati, kituo cha afya, hospitali za wilaya au mikoa." Anaongeza.

Anasema taarifa alizo nazo hata leo Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ina zaidi ya makopo 30,000 ya 'sun screen' kwa ajili ya kujikinga na athari za jua kwenye kwa ajili yao.

**WANAYAPATEJE?**

Mfamasia Mkuu wa Serikali anawataka wenye ualbino wajitokeze, pia wazazi na walezi wenye watoto wanaoishi na hali hiyo watoe taarifa zao ili watambulike, iandaliwe orodha na bajeti ya mahitaji yao iwasilishwe serikalini ili waanze kupata mafuta maalumu.

Msasi anasema walioko vijijini wawasilishe taarifa za idadi ya wanaoishi na ualbino kwa ofisi ya ustawi wa jamii, kisha ofisi ya kijiji na pia wanaoishi mijini wazifikishe deski la ustawi wa jamii na serikali mitaani ili wafahamike idadi yao na taarifa zifike kwa mkurugenzi wa wilaya au wa manispaa pamoja na mganga mkuu wa wilaya ili kuagiza mafuta hayo na wapewe bila kulipia.

Anasema wenye ualbino, washirikiane na viongozi wa vijiji, mitaa, ustawi wa jamii na viongozi hao wafikishe taarifa wilayani ili kuandaa bajeti na idadi ya mafuta wanayohitaji ili yaagizwe MSD wapatiwe tiba bure. Anakumbusha kuwa dawa hizo zinazalishwa nchini na zinapatikana kwa urahisi hivyo kila mmoja atimize wajibu wake.

**HISIA ZAO**

Mjasiriamali Mohamed Rashid, anayejishughulisha na kuuza maji maeneo ya Chanika wilayani Ilala ni miongoni mwa watu wanaohitaji mafuta kutokana na kuishi na ualbino.

Rashid maarufu kama 'Mudi' anasukuma mkokoteni juani kuuza maji kijijini Buyuni ili kupata kipato kwa ajili yake na mkewe Tatu Mforo pamoja na binti yao ambao wanaishi na hali kama yake.

Anasema anafahamu changamoto za kufanyakazi juani, lakini hana namna bora zaidi ya kupata kipato, hivyo pamoja na kushukuru jitihada za serikali kuwapa mafuta kinga ana ombi zaidi. Anaomba pia albino wafikiriwe kwenye ajira au uwezesha wa kundi maalum, ili kuepusha kufanyakazi kwenye mazingira hatarishi hasa ya jua kali kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Familia ya Rashidi, Tatu na binti yao pamoja ni miongoni mwa wanachama wa Umoja wa Kusaidiana Walemavu Chanika na Buyuni (UKWACHA) kinachoundwa wenye ulamavu wa vijiji vya Buyuni na Chanika wilayani Ilala mkoa wa Dar es Salaam.

Wanaziomba taasisi za kushughulikia wenye ualbino kama Under the same sun, (UTTS), Chama cha Albino Tanzania (TAS) kuwafikia na kuwaunga mkono kwenye juhudi za kuboresha maisha yao kwa kuwaondoa kwenye ajira hatarishi.

"Ninaweza kuuza maji nikawa salama iwapo nitapata tangi lenye lita 5,000 la kuyahifadhi. Nikapata na fedha za mtaji za kuyanunua. Nitayauza nikiwa nyumbani na wateja wakayafuata kwa ndoo na mikokoteni. Baada ya biashara kusimama nitakuwa nina nafuu kuliko hivi ninavyofanya sasa kuzunguka na mkokoteni juani mchana kutwa." Anasema Rashid.

INAENDELEA UK.13

ELIMU

NA JENIFER GILLA

# Corona ilivyomaliza kiuchumi wanawake wawekezaji utalii

NI msimu wa kiangazi kwa mikoa mingi ya Tanzania na ndicho kipindi cha mavuno kwenye sekta ya utalii, kwa vile ni muda ambao watalii humiminika kwa wingi nchini kutembea vivutio mbalimbali.

Moja ya maeneo vinara kupokea watalii ni Moshi mkoani Kilimanjaro, katika kipindi hiki unakutana na watalii wengi wanaotembelea huku na kule kuvifurahia vivutio murua vinavyopatikana eneo hilo ukiwamo Mlima Kilimanjaro.

Ni saa 10 jioni Nipashe inakutana na Magreth Shoo, nje ya duka la kuuza vifaa vya utalii, sura yake imejaa majonzi na kukata tamaa inaashiria kuna jambo linamtatiza.

Baada ya kusalimiana na kuongea machache anaanza : "Hali ni mbaya, hapa ninavyokwambia tuna miezi takribani miwili sijauza kitu katika duka hili, wala hatujapokea mtalii aliyetembelea mradi wetu." Anasema kwa huzuni.

Anaelezea kwa uchungu kuwa soko la utalii limekuwa gumu kipindi hiki tofauti na zamani, hali inayopelekea maisha kuwa magumu na kuelekea kukwamisha mustakabali wa elimu ya watoto wake.

"Kwa kweli hali hii ikiendelea hadi mwakani sielewi nitaishije na wanangu, maana hata kula yenyewe inaanza kusumbua, mategemeo yangu makuu ni kwa watalii lakini sasa matumaini si mazuri," anasema Magreth.

Mama huyo mwenye watoto wawili wanaosoma shule ya msingi, ni mmoja kati ya wanawake 18 ndugu waliounda kikundi cha mradi wa utalii kinachojulikana kama Nkweshoo Cultural Tourism katika kijiji cha Nkundoo kwenye kitongoji cha Nkweshoo, wilayani Hai mkoa wa Kilimanjaro.

Mbali na kuuza bidhaa za kitalii kama vile, vinyago, bangili, mifuko na nguo, huwatembeza watalii kwenye mapango ya asili, kuwazungusha katika kijiji chao kuona maisha halisi ya Wachaga, pamoja na kuwapeleka kwenye mashamba kujifunza kilimo cha ndizi na kahawa.

Halikadhalika huwapikia na kuwauzia vyakula vya asili kama kinywaji cha kahawa, ndizi, mtori, kiburu, ngararimu, viazi vitamu, vikuu, magimbi na vinginevyo.

Mwenendo wa ujaji wa watalii nchini umepungua na ujio wao mjini moshi ni tofauti na ilivyokuwa imezoeleka. Tatizo kuu ni janga la corona duniani unaozuia watalii kutoka nchi zao kutembelea Tanzania.

Ujio wa COVID 19 Machi 2020 pia



Watalii wakifurahia vivutio vya utalii Mlima Kilimanjaro. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa kweli hali hii ikiendelea hadi mwakani sielewi nitaishije na wanangu, maana hata kula yenyewe inaanza kusumbua, mategemeo yangu makuu ni kwa watalii lakini sasa matumaini si mazuri.




ulisababisha kusitishwa kwa muda shughuli za utalii. Japokuwa Tanzania imetangaza kuushinda ugonjwa huo lakini bado hali ya watalii ni ya kusuasua na kusababisha miradi mingi kukwama kwa muda sasa.

Mratibu wa Mradi Nkweshoo Cultural Tourism, Stella Shoo, anasema mara ya mwisho kupokea watalii ilikuwa ni Oktoba mwaka jana na walikuja wanane , Ogosti walipokelewa watalii 12 hali ambayo ni tofauti na kabla ya kuwapo janga la corona ambapo walikuwa wakipokea watalii zaidi ya 30 kwa mwezi.

Hali hiyo ya kusuasua kwa watalii imesababisha kukosekana kipato cha kutosha cha kuendesha mradi hali inayowakatisha tamaa, kama anavyoelezea mweka hazina wa mradi huo, Aneth Shoo.

"Kabla ya kutokea kwa janga la virusi vya corona, kwa mwezi tulikuwa tukipokea watalii wasiopungua 30, hivyo ukitoa gharama za kuendesha mradi hela tuliokuwa tukiweka benki kila mwezi ni Sh.400,000 hadi 600,000, lakini kwa sasa benki kuna Sh. 50,000 .

"Tumepata hasara, kama unavyoona duka hilo limejaa bidhaa tulizotegemea kuuza msimu wa watalii, pesa yote ya mradi tulinunua bidhaa hizo, hapa tupo weupe, tunategemea labda mwakani tutaweza kuuza." Anasema Aneth.

Halikadhalika, kutokupata mapato ya kutosha ya kuendesha kikundi hicho kumesababisha shughuli za maendeleo na kijamii walizokuwa nazo kuyumba ndani ya kikundi na mtu mmoja mmoja.

Kwa mujibu wa Ofisa Masoko wa mradi huo, Edith Shoo, wameshindwa kusomesha watoto yatima takribani 18 ambao wazazi wao wamefariki na VVU kutokana na kukosa pesa za mradi huo.

Katika kupambana na hali ya kudhorota kwa shughuli za utalii, mratibu wa miradi kutoka Bodi ya Utalii Tanzania, Elirehema Mturo, anasema wamekuwa wakiwashauri wanawake kujihusisha na shughuli nyingine za kiuchumi badala ya utalii.

Kwa mujibu wa mratibu miradi huyo, wanawapa mawazo ya kufanya shughuli nyingine za kitamaduni za kujiingizia kipato kama vile kilimo cha kahawa, ufugaji, na nyinginezo ili kuwa na njia mbadala ya kujiingizia kipato na kuepuka kutegemea utalii peke yake.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UN WTO) ya mwaka 2020, inayozungumzia athari za COVID-19 kiuchumi katika sekta ya utalii, linakadiria upotezaji wa dola milioni 850 hadi bilioni 1.1 zitokanazo na kuwasili kwa watalii wa kimataifa.

Dola milioni 910 hadi trilioni 1.1 katika mapato ya kuuza nje na ajira milioni 100-120 duniani ikiwa mipaka ingefunguliwa Julai, Septemba au Desemba 2020.

Ripoti hiyo pia ilielezea kuwa katika nchi nyingi zinazoendelea na zilizo na maendeleo duni utalii hutoa fursa ya ajira hasa kwa wanawake, vijana walio chini ya miaka 35. Hivyo basi wanawake wasio na ujuzi, pamoja na vijana, wanaathiriwa kwa kiasi kikubwa kwa kupunguzwa kwa kazi katika sekta ya utalii kutokana COVID-19.

Wakati huo huo takwimu za baraza la kimataifa la safari na utalii zinaonyesha kuwa idadi ya watalii Afrika Mashariki inatarajiwa kuongezeka kufikia milioni 134 mwaka 2030 wakati nchi zinazotegemewa kupata wageni wengi ni Tanzania, Rwanda na Uganda, huku wanawake wakionekana wana nafasi kubwa ya kunufaika zaidi na na sekta hiyo.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Gitanjali Rao mwanasayansi kinda aliyetikisa dunia 2020

MTOTO wa mwaka ndiyo sifa anayopewa binti wa miaka 15 Gitanjali Rao ambaye anamaliza mwaka 2020 kwa kuahidi kutatua matatizo ya dunia.

Msichana huyo mwanasayansi na mvumbuzi aliyetangazwa kama Mtoto wa Kwanza wa Dunia wa mwaka 2020, tayari amefanya makuu na amevumbua teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifaa kinachoweza kubaini uwepo wa sumu kwenye maji na app au programu ya mtandao inayotambua uonevu wa mtandaoni.

Gitanjali anasema kuwa anatumaini atawahamasisha wengine kubuni mawazo ya "kutatua matatizo ya dunia kwani kama ameweza kwanini usiweze".

Gitanjali Rao, alichaguliwa miongoni mwa watoto zaidi ya 5,000 waliokuwa wameteuliwa kugombea nafasi ya Mtoto wa mwaka 2020.

"Kama ninaweza kufanya uvumbuzi, hata wewe au mtu mwingine unaweza pia kuufanya na nina imani yeyote anaweza kuvumbua," anasema.

Katika mahojiano na jarida la Time Magazine na mwigizaji na Angelina Jolie, Gitanjali, anasema kuwa hafanani na "mwanasayansi halisi.'

"Kila kitu ninachokiona kwenye televisheni kiko hivyo, kwa kawaida utawaona Wazungu wanaume ndiyo wanasayansi," anasema.

"Lengo langu limegeuka kwa kweli si tu kuanzia kubuni kifaa changu binafsi kwa ajili ya kutatua matatizo ya dunia, bali kuwahamasisha wengine kufanya niliyofanya pia. Kwasababu, kutokana na uzoefu wangu binafsi, si rahisi kuamini unapokosa kumuona mtu mwingine anayefanana na wewe."

Gitanjali kutoka Jimbo la Marekani la Colorado, anasema kuna matatizo mengi yanayohitaji kutatuliwa.



Gitanjali Rao akiwa maabara kugundua kifaa kilichotambua uwepo wa risasi kwenye maji huko Florida. **PICHA: MTANDAO**

"Kizazi chetu kinakabiliwa na matatizo ambayo hayakuwahi kushuhudiwa miaka ya nyuma. Lakini wakati huo huo, tunatatizwa changamoto ambazo zilianza zamani na ambazo bado zipo," analiambia jarida la Time Magazine.

"Kwa mfano, tupo katikati ya janga la dunia na wakati huo huo, bado tunakabiliwa na matatizo ya haki za binadamu. Kuna mambo ambayo hatukuyasababisha, lakini ambayo tunahitaji kuyatatua sasa, kama vile mabadiliko ya tabianchi na uonevu wa kimtandao yaliyoletwa na teknolojia."

Tuzo ya Time Magazine ya hivi karibuni itatolewa kwa Gitanjali Rao.

Awali msichana huyo alitangazwa kama "mwanasayansi wa kwanza wa Marekani aliye na umri mdogo zaidi" kwa kuvumbua kipimo cha haraka na cha rahisi cha kupima maji machafu.

Time Magazine ilianza kwa kumtangaza mwanaume wa mwaka 1927 na baadaye ikamtaja mtu wa mwaka.

Gitanjali alitangazwa kuwa mwanasayansi bingwa mtoto wa Marekani mwaka 2017, alipogundua kifaa cha 'Tethys' kinachotumiwa kubaini uwepo wa sumu ya madini ya risasi kwenye maji kazi aliyoifanya mwaka 2017.

Akiwa darasa la saba wakati huo aligundua kwa kipindi kifupi cha miezi mitano kifaa cha kubaini uwepo wa risasi kwenye maji baada ya jiji hilo kusumbuliwa na uwepo sumu za madini hayo kwenye maji.

Katika Jiji la Flint lililoko Michigan mwaka 2014, chanzo chake cha maji kilichafuliwa na madini hayo na kuhatarisha maisha.

> Gitanjali Rao, alichaguliwa miongoni mwa watoto zaidi ya 5,000 waliokuwa wameteuliwa kugombea nafasi ya Mtoto wa mwaka 2020.

**ALICHOFANYA GITANJALI**

Wakati huo akiwa na miaka 11 aliguswa na tatizo la watu kunywa maji machafu yenye madini tembo (heavy metal) hasa lead au risasi na kutengeneza kifaa hicho cha gharama nafuu kilichobaini uwapo wa madini hayo majini.

Ugunduzi huo umewafikisha mahakamani watendaji wengi wa mamlaka ya maji na ulibainisha kuwa Marekani yenye vyanzo vya maji karibu 5,000 vingi vilikuwa na risasi.

Athari za madini ya lead ni nyingi na mojawapo ni kusababisha anemia au upungufu wa damu, maradhi ya figo, huathiri ubongo na iwapo watu watatumia madini hayo kwa kiwango kikubwa yanaweza kuwaua.

Wakati mwingine inahusishwa na kuharibika mimba kwa vile mjamzito anapokula vyakula au kunywa maji yenye madini hayo yanavuruga ukuaji wa mtoto aliye tumboni na kuharibu mfumo wake wa mishipa ya fahamu.

Baadhi ya vifaa vinavyotengenezwa na lead au risasi ni pamoja na vifaa vya umeme kama nyaya na taa zake.

Mwaka jana, Greta Thunberg, mwanafunzi wa kike kutoka Uswiss ambaye alihamasisha vuguvugu la dunia la mapambano ya mabadiliko ya hali ya hewa, alikuwa mtu mwenye umri mdogo zaidi kuchaguliwa na jarida hilo.

Time Magazine inasema kuwa mtoto mpya wa mwaka ni "kipimo cha viongozi wadogo wanaoibukia wa kizazi kijacho cha Marekani ".

Jarida hilo linajiandaa kumtangaza mtu wake wa dunia mwaka 2020 wiki ijayo.

**BBC SWAHILI**

# Wenye ualbino wakizingatia haya, watazilinda ngozi zao

**INATOKA UK.11**

Katibu wa UKWACHA, Amina Kisembe, anasema umoja huo una wanachama wanne wanaoishi na ualbino ikiwamo familia ya Mohamed Rashid na kijana mwingine ambaye ni mjasiriamali.

Aidha, anaeleza kuwa wanachama hao wanajituma kufanyakazi za kujikimu akiwaomba wadau mbalimbali kuwasaidia na kuwaunga mkono kwenye jitihada wanazofanya za kuboresha na kuinua maisha yao.

**MIONZI KUATHARI NGOZI**

Mionzi ya UV inaelezwa na mitandao ya afya kuwa chanzo cha saratani ya ngozi.

Kadhalika, inatajwa kuwa huunguza ngozi na kusababisha wekundu ujulikanao kama 'sunburn' hasa usoni .Mionzi hii ni chanzo cha kuichakaza ngozi na kuifanya kuwa na makunyanzi na mikunjo. Ikiingia machoni husababisha yawe mekundu, huchangia kuota mtoto wa jicho (cataracts) kuweka ukungu kwenye kioo au lenzi ya jicho hatimaye upofu au uoni hafifu.

Mitandao ya afya ukiwamo wa 'American Cancer Society' unasema iwapo mtu atakuwa katika mazingira ya kuchomwa sana na mionzi ya UV, anadhoofika kinga ya mwili na kumsababishia maradhi yakiwamo yasiyoambukiza.

**KUJIKINGA NA UV**

Kwa watu weupe zaidi na wanaoishi na ualbino wanashauriwa kutumia mafuta au 'sun screen' yenye kiwango kikubwa cha kuzuia mionzi, pia waepuka jua kali na kama wanalazimika kufanyakazi wakati huo wakae kwenye kivuli hata kama kuna joto wahakikishe wanakwepa jua la moja kwa moja.

Mavazi ya kufunika mwili ni muhimu kufunika uso, shingo, macho, mikono na miguu na kutumia kofia kuziba kichwa na miwani kuzuia mionzi machoni na sehemu zinazozunguka uso.

ELIMU

**NA MARCO MADUHU, KISHAPU**

# Wazoefu maisha vijiweni walipogeuka wakulima stadi



Baadhi ya vijana wa Kijiji cha Mipa wilayani Kishapu wakiwa kazini. **PICHA: MARCO MADUHU**

VIJANA waishio maeneo mengi vijijini asilimia kubwa huendesha maisha yao kwa kutegemea kilimo ukiwamo pia ufugaji, kazi wanayoifanya msimu wa mvua.

Lakini wanabaki na changamoto moja na msimu wa mvua unapokwisha hawana kazi za kufanya mashambani na idadi kubwa hasa ya wasio na mifugo hukaa vijiweni maarufu kama 'senta'.

Wapo baadhi wanaojitumbukiza kwenye starehe wakitumia fedha walizovuna msimu wa kilimo na zinapomalizika wanaendelea kuwa na maisha duni.

Kutokana na ukosefu huo wa kipato cha uhakika na namna bora ya kujiajiri, Shirika la Tanganyika Christian Refugee Services (TCRS), linalojihusisha na utunzaji wa mazingira na upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo kame, limewaona vijana hao.

Limewaanzishia mradi wa kilimo cha umwagiliaji mboga, anasema Mwanamina Jumanne, Ofisa Miradi wa TCRS.

Anaongeza kuwa wameanzisha mradi wa kilimo cha mboga cha umwagiliaji, katika Kijiji cha Mipa kilichoko kata ya Sekebogolo wilayani Kishapu na tayari vijana 200 wananufaika.

> "Maji wanayotumia ni ya visima na malambo, ila kazi ya kumwagilia inaanza kuanzia Mei kwa sababu masika inamalizika.

Wameanza na kikundi cha vijana 200 waliopatiwa elimu ya kilimo cha kisasa, mbegu za mboga mbalimbali zikiwamo spinachi, karoti, nyanya, vitunguu, mchicha, mbolea, pamoja na miundombinu ya kumwagilia kwa njia ya matone (drip irrigation) ili kutunza maji, anasema Mwanamina.

"TCRS tuna lengo la kutatua tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wa maeneo ya vijijini, hasa pale msimu wa mvua unapokwisha ili wasirudi vijiweni bila kazi na kuendelea kuwa na maisha magumu," anasema Ofisa Miradi.

"Tunaamini kilimo hiki cha umwagiliaji kitabadili mfumo wa maisha ya vijana hawa, sababu watakuwa wakifanya kazi muda wote na kujipatia kipato kitakachowainua kiuchumi," anaongeza.

Frank George ambaye ni msimamizi wa mradi huo wa umwagiliaji wa mboga kwa vijana hao 200 wa Mipa, kutoka shirika hilo anasema wanawahudumia vijana katika vijiji vya Mwamasololo na Durisi lengo ni kupunguza tatizo la ajira kwa vijana pamoja na kuwainua kiuchumi.

Mwenyekiti wa kikundi cha vijana hao Fortina Boniface, anasema baada ya kupewa elimu hiyo kilimo cha umwagiliaji cha mboga, maisha ya vijana kwa sasa yamebadilika kutokana na kujipatia kipato.

Anasema wanalima spinachi, kabichi na nyanya zinazouzwa kwenye masoko mbalimbali ya ndani kwa sababu wafanyabiashara wa nboga huwafuata mashambani kununua bidhaa hizo.

Anasema maji wanayotumia ni ya visima na malambo, ila mvua kazi ya kumwagilia inaanza kuanzia Mei kwa sababu masika inamalizika.

Hata hivyo kutokana na mabadiliko ya tabianchi mara nyingi mvua hazitabiriki mfano kwa sasa mvua za vuli zimeanza kunyesha mwishoni mwa Desemba.

Boniface anasema hapo awali walikuwa wakiishi maisha magumu kutokana na kutokuwa na vyanzo vya mapato, lakini baada ya kupewa maarifa hayo mfumo wa maisha yao umebadilika, na siyo tena watu wa kwenda kukaa vijiweni bali muda wote wanashinda mashambani.

"Tunashukuru TCRS kwa mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji cha mboga pamoja na vifaa vya kumwagilia tunaamini kazi inabakia kwetu ili maisha yetu yabadilike kiuchumi. Tuko vizuri tofauti na hapo awali," anasema Boniphace.

"Mradi huo wa umwagiliaji ungekuja zamani, maisha yetu vijana wengi wa hapa kijijini tungekuwa na maendeleo zaidi kwa sababu tulikosa kujua namna bora ya kujiajiri wenyewe kupitia kilimo," anaongeza.

Diwani wa Kata ya Sekebugolo Ferdinand Mpogomi, anawataka vijana wanachama wa mradi huo kujua kuwa fedha wanazozipata ni za kuwatumia kufanya maendeleo na siyo kwenda vijiweni kustarehe.

Anasema katika maeneo ya vijijini kume kuwapo na kawaida ya vijana wakishapata pesa hawaonekani ni kwa vile wanakimbilia mijini kwenye starehe na pesa zikiisha hurudi vijijini na kuendelea kuishi maisha magumu kama zamani.

"Naombeni sana vijana pesa ambazo mnazipata kwenye kilimo hicho cha mboga, msiendekeze starehe bali zitumieni kujenga vyumba za kisasa na hata kufungua miradi mingine kumbukeni hii ni fursa ambayo mmeipata itumieni kikamilifu kujikwamua," anasema Mpogomi.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Joseph Swalala, anatoa wito kwa vijana hao ambao wamewezeshwa kupitia kilimo cha umwagiliaji mboga, kuomba mkopo Halmashauri kwavile kuna asilimia 10 yafedha zinazotengwa ili wapanue wigo wa mashamba yao.

"Natoa wito kwa vijana hawa 200 kupitia kikundi chao, waandae katiba kisha kuja kuomba fedha za vijana za halmashauri, tunazozitoa bila riba asilimia nne kwa vijana, nne kwa wanawake, mbili kwa walemavu, ili wapanue uwekezaji na kupata masoko makubwa ya kuuza mboga," anasema Swalala.

Aidha anasema vijana wengi wamekuwa wakilalamika kuwa hawana ajira, na wakati kuna fursa nyingi ambazo wanaweza kuzitumia kujiajiri wenyewe, ambapo kwenye suala la upataji wa mitaji fedha zipo za halmashauri, na kubainisha kuwa wanachopaswa kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali vinavyowawezesha kupata fedha hizo.





## Wataka tamasha la mvinyo, zabibu

Na Renatha Msungu, DODOMA

WADAU wa zabibu na mvinyo mkoani Dodoma wametaka kuwe na tamasha la matangazo zaidi ya mazao hayo ili kuvuta uwekezaji na tija kwenye sekta hiyo.

Peter Mavunde kutoka baraza la wazee la mkoa wa Dodoma, alitaka mkoa huo kuwa na mkakati wa kutangaza fursa zilizopo katika zabibu na mvinyo ili wawekezaji wengi wajitokeze.

Aidha, alitaka kuanzishwa maonyesho hayo ili kutangaza mvinyo na zabibu kusaidia kuufikia na kupatikana kwa masoko na wawekezaji. Halikadhalika akizungumzia sekta hiyo, Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, alisema kumekuwa na changamoto kwenye soko la zabibu za wakulima licha ya serikali kuondoa ushuru kwenye uchuuzi wa zabibu, viwanda vingi vinaagiza unga wa zabibu kutoka Afrika Kusini.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliziagiza halmashauri zote kupanda miti ya matunda kama korosho, maembe na zabibu kukuza afya na uchumi wa wananchi.

Akizungumza hivi karibuni katika kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa (RCC) ambacho pamoja na kilimo cha zababu kilizungumzia masuala mengine kadhaa, alioongeza kuwa ni muhimu kwa halmashauri kuhamasisha wananchi kupanda miti yenye tija kiuchumi.

"Hata mashamba yaliyopo yasimamiwe, eka moja unapanda wastani wa miche ya mikorosho 33 na ukivuna unapata kilo 40 huo ni uchumi mkubwa sana ni lazima kuwaambia wananchi wetu kuchangamkia fursa kama hizi," alisema Mkuu wa Mkoa.

Katibu Tawala Msaidizi Sekta ya Uchumi mkoani Dodoma, Aziza Mumba, akieleza hali ya kilimo alisema mkoa huo una hekta milioni 4.13 kati ya hizo zinazofaa kwa kilimo ni milioni 2.23 sawa na asilimia 54 ya eneo lote.

Pia alisema mkoa una hekta 50,457 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini ni 17,947 pekee zinazomwagiliwa wakati wa msimu wa mvua na nyingine 4,710 zinazolimwa kipindi cha kiangazi.

Akizungumzia upatikanaji wa chakula, alisema hali ya upatikanaji ni nzuri na kutaja baadhi ya matarajio katika wilaya akisema kwamba malengo ya uzalishaji mazao kwa msimu wa mwaka 2020/2021 ni pamoja na tani 163,332 za mazao ya chakula na tani 42,504 za mazao ya biashara zitakazozalishwa wilayani Bahi.

Alisema Chamwino inategemea kuzalisha tani 131,589 za mazao ya chakula wakati tani 52,520 ni za mazao ya biashara.

Aliongeza kuwa Chemba inatarajia kuzalisha tani 182,641 za mazao ya chakula na tani 160,260 za biashara wakati Dodoma Mjini inatarajia kuzalisha tani 48 ,201 za mazao ya chakula na tani 53,109 za mazao ya biashara.

# Wakumbushwa kuwa wasafi msimu wa mvua

Na Peter Mkwavila, DODOMA

> **"Niwaombe wakazi wa Jiji la Dodoma, wenye hoteli, migahawa na mamalishe, wauza vyakula na mboga kuchukueni tahadhari ya kujiweka katika mazingira safi huku mkihakikisha mnanawa kwa sabuni muda wote," alisema.**

OFISA Afya Jiji la Dodoma, Abdalah Mahia, amewataka wamiliki wa hoteli na migahawa kuzingatia usafi kipindi chote hasa wakati huu wa mvua za masika, kuepuka magonjwa ya mlipuko yakiwamo kipindupindu na homa ya matumbo.

Mahia, alitoa agizo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa kunawa na kuzingatia usafi na kuwataka wamiliki wa hoteli, migahawa na mamalishe kuweka tahadhari ili kujiepusha na magonjwa ya milipuko ambayo yanayoweza kujitokeza kutokana na uchafu wa mazingira.

Aliwataka kila mmoja kuwa na utamaduni wa kunawa maji tiririka na sabuni kila wakati hata kama corona umetoweka ili kujilinda na maradhi mengine ya milipuko.

"Niwaombe wakazi wa Jiji la Dodoma, wenye hoteli, migahawa na mamalishe, wauza vyakula na mboga kuchukueni tahadhari ya kujiweka katika mazingira safi huku mkihakikisha mnanawa kwa sabuni muda wote," alisema.

Alisema kila mtu anatakiwa anawe kwa ajili ya kujilinda na magonjwa ya kuambukiza kwa kufuata kanuni za unawaji wa mikono.

Aidha, alisema halmashauri hiyo inaendelea kufanya msako wa wamiliki wa nyumba ambao hawazingatii kanuni za afya na wakati mvua zinaponyesha hufungulia mabomba ya maji taka na kuyatiririsha kwenye mtaro ya maji na kuzagaa barabarani.

Aidha, ofisa huyo aliwataka wakazi wa Dodoma, kuwa na vyoo bora vya kisasa na kuondoka na vile vya muda mfupi ambavyo vimekuwa vikianguka kipindi cha mvua.

Aliongeza kuwa takwimu zinaonyesha kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuondokana na magonjwa ya uchafu hasa wakati wa mlipuko wa corona.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, akiangalia eneo la Hospitali ya Rufani ya Uhuru litakalopitiwa na miundombinu ya maji kutoka tangi la maji lililoko eneo la Buigiri wilayani Chamwino, alipofanya ziara ya kikazi jijini Dodoma. **PICHA: HAPPY SHAYO**

# Wananchi wataka uwazi zaidi urasimishaji ardhi

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Ndachi, Kata ya Mnadani, wameitaka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuweka wazi ramani na mikataba ya makandarasi wapima ardhi wanaoshiriki kwenye kazi ya umilikishaji ardhi kwa wananchi.

Hayo, yalibainishwa juzi na baadhi ya wakazi walioshiriki mkutano wa urasimishaji uliofanyika mtaa wa Matuli, Kata ya Mnadani, Dodoma.

Katika mkutano huo wananchi walidai kukosekana uwazi katika kazi hiyo kumekuwa sababu kuu ya ukiukwaji wa makubaliano ya mkutano uliofanyika awali baina yao na Halmashauri ya Jiji Dodoma.

George Mwimbe, kutoka Matuli, aliiomba halmashauri kuweka wazi ramani na mikataba ya makandarasi wa upimaji ardhi ili kuondoa vitendo vinavyosababisha ukiukwaji wa makubaliano baina yao na wananchi. Alisema lengo la kutaka kuwekwa wazi kwa ramani ni kusaidia wananchi wa eneo hilo kufahamu sehemu wanazomiliki.

"Tunataka kuonyeshwa ramani ili kuelewa nani yupo wapi na kapitiwa na barabara ipi ili kusiwepo na kudhulumiwa maeneo yetu na kampuni ya upimaji wa ardhi wakati wa urasimishaji ardhi," alisema Mwimbe.

Alfred Isaac, mkazi wa eneo hilo alisema kuwa jiji linatakiwa kuzingatia maoni yao ili kuondoa maswali ambayo yamekuwa yakijitokeza kwa wananchi kutokana na kuficha ramani za maeneo pamoja na mikataba ya makampuni yaliyopewa kazi za upimaji wa maeneo yao.

Aidha, wakazi hao walibainisha kuwa kukosekana imani na zabuni iliyotolewa kwa mkandarasi wa upimaji ardhi katika kata hiyo.

Hatua hiyo ilimwinua Ofisa Mipango Miji wa Jiji la Dodoma, Aisha Masanja, na kulitolea ufafanuzi kuwa hakuna makubaliano ambayo yatakiukwa kila kitu kitakwenda kama walivyokubaliana katika mikutano ya awali.

Alisema, kuwa kitendo cha wakazi hao kutaka kampuni inayopima ardhi kuwekwa bayana ili wao wachague ipi wanaihitaji kufanya nayo kazi jambo hilo halitawezekana kwa mujibu wa kanuni.

"Suala la kupata zabuni ni kampuni zinaleta maombi yao kwa jiji na siyo wananchi kuzipitisha kwani wakipitisha wao wanaweza kuwa ni sehemu ya kuharibu mradi, hivyo basi jukumu la kupitisha kampuni litakuwa chini ya jiji," alisema Masanja.

Aidha, Diwani wa Kata ya Mnadani, Paulo Richard, alisema kuwa ataendelea kuufuatilia mvutano huo baina ya wakazi wa eneo lake na uongozi wa Jiji la Dodoma ili kupatikana kwa suluhu ya kero hiyo.

Kazi ya umilikishaji ardhi katika mtaa wa Matuli, kata ya Mnadani inatarajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia wiki hii.



HABARI MBEYA

# Walalama jinsi mtaro unavyowaangamiza

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKAZI wa Nzovwe wilayani Mbeya, wameiomba serikali kujenga mtaro mkubwa wa maji unaopita katika maeneo yao kuwaepusha na mafuriko yanayotikisa eneo hilo kila wakati, yakisomba watu na kubomoa nyumba zao.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya ilipozuru Kata ya Nzovwe ikijumuisha maofisa wa Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS) na wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Mwenyekiti wa kamati hiyo, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alitembelea eneo hilo baada ya nyumba mbili kubomolewa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Mmoja wa wananchi, Selina Sanga, aliyeathiriwa na mafuriko aliwaambia wajumbe kuwa mafuriko hayo yalitokea muda ambao walikuwapo nyumbani hivyo wakafanikiwa kuokoa mali zilizokuwamo ndani licha ya kwamba nyumba ilibomoka, hakuna aliyeumia.

"Siku zingine watoto walikuwa wanabaki peke yao hapa, lakini safari hii tulikuwapo, pengine wangekuwa peke yao nyumba ingewaangukia, tunamshukuru Mungu hata mali zetu hazikuharibika sana," alisema Selina.

Maximilian Schone, alisema madhara ya mafuriko kwenye makazi yao yanatokea kila mwaka kutokana na mfereji huo akidai kuwa baadhi ya watu wameyahama makazi yao kutokana na hofu.

Diwani wa Kata hiyo, David Mwashilindi alisema mwaka jana watoto wawili walifariki dunia baada ya kusombwa na maji ya mfereji huo hali inazidisha hofu kwa wananchi.

Aliiomba serikali iwasaidie kudhibiti maji hayo, ili wananchi wawe salama na waendelee na shughuli zao kwa amani na utulivu tofauti na ilivyo sasa ambako alidai wazazi wanaacha shughuli zao na kuwahi nyumbani wanapoona dalili za mvua.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Ntinika aliwaagiza maofisa wa TANROAD na TARURA, kukaa pamoja na kulitafutia tatizo hilo ufumbuzi wa kudumu.



Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakisafiri kwa kutumia trekta katika kijiji cha Ilongo Kata ya Mahongole juzi, usafiri ambao wanautumia kwenda mashambani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 'Ukibainisha wezi unalamba bingo'

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

KATIKA jitihada za kukomesha biashara haramu ya madini, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, itaanza kutoa zawadi ya pesa taslimu kwa yeyote atakayetoa taarifa zitafanikisha kukamatwa watuhumiwa wanaojihusisha na utoroshaji wa madini.

Mkuu wa Wilaya, Mayeka Saimon, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao maalumu na vyombo vya ulinzi na usalama vya wilaya pamoja na Maofisa wa Madini wa Wilaya, kilicholenga kujadili namna ya kukomesha kutorosha madini.

Kikao hicho kilifanyika ikiwa ni wiki chache tangu polisi wawili na mfanyabiashara kukamatwa kwa tuhuma za kuhusika na utoroshaji wa madini na kufikishwa mahakamani.

Hatua hiyo, ilifuatiwa na Wizara ya Madini kuwafutia leseni baadhi ya wafanyabiashara wa dhahabu wilayani humo.

Saimon alisema zawadi hiyo itatolewa kwa wote kuanzia askari, raia wa kawaida na wachimbaji wadogo ili kudhibiti utoroshaji huo wa madini unaichafua wilaya hiyo.

Vilevile aliwataka wananchi hao kutoa taarifa hata za wanunuzi wa dhahabu wanaonunulia madini hayo maeneo yasiyo rasmi kama nyumbani kwa vile ni kinyume cha sheria.

"Tukiletewa taarifa, tukafuatilia na kuthibitisha pasipo shaka na mhusika kukamatwa, tutatoa zawadi kwa mtoa taarifa hii zawadi haitabagua mtu," alisema Simon.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Chunya, Titus Lugomba, alisema atachukua hatua za kudhibiti polisi wasihusishwe na utoroshaji wa madini, baada ya wale wa awali kukamatwa.

Aliahidi kuitisha kikao na maaskari wote wa wilaya hiyo ili kutoa maelekezo na kukemea vitendo ambavyo haviendani na maadili ya jeshi ikiwamo kushiriki kwenye utoroshaji madini.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Chunya, Sabai Nyansiri, alisema tangu soko la madini lilipoanzishwa wilayani Chunya, uzalishaji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo, ulieongezeka zaidi ya mara 10 na hivyo ufanisi wa soko unaonekana.

Alisema tatizo lililopo ni baadhi ya maeneo kuwa na udhibiti mdogo wa utoroshaji wa dhahabu hali inayohitaji ushirikiano wa wadau wote wa madini hayo kwenye kudhibiti ili yote yauzwe kwenye soko rasmi.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa soko hilo uzalishaji wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wilayani humo ulikuwa kilo 20 kwa mwezi lakini kwa sasa umefikia zaidi ya kilo 200 kwa mwezi.

Baadhi ya askari walieleza baadhi ya mianya inayosababisha utoroshaji wa madini wilayani humo na namna ya kudhibiti.

Mmoja wa askari hao, Abuu Mchuchuli, alisema hakuna utaratibu wa kuthibitisha kiwango kinachozalishwa kwenye machimbo na kiasi halisi kinachofikishwa sokoni na kwamba mazingira hayo yanaweza kuwa chanzo cha utoroshaji.

# Wazembe RUWASA kufuatiliwa, kutumbuliwa

Na Nebart Msokwa, MBARALI

MBUNGE wa Viti Maalumu Mbeya, Suma Fyandomo, ameahidi kufuatilia miradi ya maji mkoani humo ambayo maofisa wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), wameagizwa na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, kuikamilisha kabla ya Machi mwaka huu.

Naibu Waziri wa Maji alifanya ziara ya siku tano katika halmashauri sita kati ya saba za Mbeya alizotembelea zaidi ya miradi 10 ambayo inaendelea kutekelezwa ikiwamo inayosimamiwa na Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) na inayosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA).

Akiwa kwenye miradi hiyo Naibu Waziri, alitoa maagizo kwa wasimamizi wa miradi hiyo kuikamilisha kabla ya wiki ya maji itakayoadhimishwa Machi mwaka huu, ili kutimiza azma ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kusogeza huduma hiyo karibu na makazi ya wananchi.

Fyandomo ambaye aliambatana na Naibu Waziri kwenye ziara hiyo, alisema atahakikisha anafuatilia utekelezaji wa maagizo hayo ili watekelezaji wasije wakabweteka na kuchelewesha miradi hiyo.

Alisema wanawake na watoto ni makundi yanayoteseka zaidi na tatizo la ukosefu wa maji kwa maelezo kuwa ndiyo wanaohangaika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

"Tuliwaaminisha kinamama wakati wa kukitafutia kura chama chetu kuwa tutamaliza kero ya maji, lakini tangu mwanzo wa ziara mpaka sasa nimebaini kuwa wataalamu wetu hasa wa RUWASA ndiyo wanaotukwamisha, hawaendi 'site' kwenye miradi huku wakiandaa taarifa za kufariji, sasa nawahakikishia kuwa nitafuatilia miradi yote aliyotoa maagizo Naibu Waziri ili kuiharakisha," alisema Fyandomo.

Awali Naibu Waziri wa Maji, Mahundi, alisema katika maeneo mengi alikerwa na utekelezaji duni wa miradi hasa inayosimamiwa na RUWASA na kuahidi kuwa watawaondoa kwenye nafasi zao mameneja wazembe na kuajiri wapya.

"Natamani tuje tuitumie wiki ya maji mwaka huu kuizindua miradi, kwahiyo hakikisheni mnafanya kazi kwa bidii, mameneja jitahidini kwenda kwenye maeneo ya wananchi na muwashirikishe wakati wa kufanya shughuli hizi," alisema Mahundi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Mbarali, Hashim Mwalyawa, alisema moja kati ya matatizo ambayo yamekuwa yakikikosesha chama hicho kura kwenye chaguzi mbalimbali ni ukosefu wa huduma ya maji.

Aliiomba serikali kushirikiana na chama hicho kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo, ili wananchi waamini kile walichoahidiwa kuwa ni kweli.



# Ahimiza ubunifu na uwajibika MAELEZO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Habari -MAELEZO Zanzibar, Omar Said Ameir, amewataka wafanyakazi wa idara hiyo, kuwa wabunifu na wawajibikaji katika kutekeleza majukumu yao.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya kumuaga aliyekuwa fundi Mkuu wa Idara ya Habari Maelezo Omar Suleiman Othman (Omar Mabomba) aliyestaafu kwa mujibu wa sheria.

Alisema Idara ya Habari Maelezo ni msemaji wa shughuli za serikali, hivyo wanajukumu la kuhakikisha wanaelezea mafanikio ya miradi inayotekelezwa na changamoto inayoikabili miradi hiyo kwa wananchi kwa wakati.

Aliwashauri wafanyakazi wa idara hiyo kubadilika kwa kuongeza nidhamu na ufanisi katika utendaji wao wa kazi ili kuendana na kasi ya serikali ya sasa kwa kuzingatia misingi ya uwajibikaji pamoja na nidhamu kazini.

Kaimu Mkurugenzi aliwakumbusha wafanyakazi wa Idara ya Habari Maelezo kwamba maofisa wote wa habari wa taasisi za serikali wapo chini yao hivyo wanawajibu wa kuwapa ushirikiano ili kufanikisha kazi zao za kuwahudumia wananchi.

Mstaafu Omar Suleiman Mabomba, akitoa nasaha na shukurani zake aliwashauri wafanyakazi kujituma zaidi na kupenda kazi pamoja na kufuata sheria na kanuni za kazi.

"Siri kubwa ya mafanikio katika kazi ni kutunza nidhamu kwa wakubwa na wadogo, kudumisha upendo ushirikiano katika kazi," alisisitiza Fundi Mkuu, anayestaafu.

Awali Ofisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Ikulu, Mwatima Rashid Issa, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu alimpongeza Omar Suleiman kutokana na uadilifu wake na kuipenda kazi yake wakati wote alipokuwa mtumishi wa umma.

Alimshukuru kwa juhudi kubwa aliyoonyesha wakati wa utumishi wake na kuwa mfano kwa wafanyakazi wenzake na aliwataka kufuata nyayo za mstaafu huyo kwa kuwa waadilifu, wabunifu na wenye nidhamu.

**"Siri kubwa ya mafanikio katika kazi ni kutunza nidhamu kwa wakubwa na wadogo, kudumisha upendo ushirikiano katika kazi," alisisitiza Fundi Mkuu, anayestaafu.**

# SMZ yataja mpango kudhibiti udhalilishaji

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imewahakikishiwa wananchi kuwa imeweka mikakati maalum kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji kwa watoto na wanawake.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akifungua tamasha la kwanza la pongezi kwa Wana Sunni Madrasa katika hafla iliyofanyika Mkunazini jana.

Akimwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi; Waziri Haroun aliahidi kukutana na wadau wanaoshughulikia vitendo vya udhalilishaji, likiwamo Jeshi la Polisi, Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu kwa lengo la kujenga mikakati ili kuharakisha usikilizaji wa kesi za makosa hayo ya udhalilisha yanayoelezwa kuwa yameshamiri nchini.

Alisema SMZ hairidhishwi na mrundikano wa kesi za udhalilishaji uliopo na hivyo akaitaka jamii kujenga ushirikiano na vyombo vya sheria ili kufanikisha mchakato wa kesi pamoja na kuondokana na muhali au kuoneana aibu.

Alitumia fursa hiyo kuwapongeza walimu wanaofundisha watoto hao kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kuwaomba kuendelea na juhudi za kuisambaza taaluma hiyo hadi vijijini Unguja na Pemba.

Katika hafla hiyo Waziri Haroun alikabidhi zawadi kwa washindi wa tamasha la 'Nasheed', ambapo mwanafunzi Nasra Abdalla Mohamed alikuwa mshindi wa kwanza na hivyo kuzawadiwa friji, mkoba pamoja na vitu vingine.

Aidha, mwanafunzi Asiat Ramadhan Jussa, alikamata nafasi ya pili na kuzawadiwa cherehani na mkoba wakati Mudrik Msellem Ali akiondoka na ushindi wa tatu na kuzawadiwa baiskeli, mkoba na zawadi nyingine.

Mapema, Katibu Mtendaji Idara ya Sensa na Sanaa, Omar Abdalla Adamu, aliwashukuru waandaji wa tamasha hilo na kusema wamekamilisha taratibu zote za kisheria na kufauta mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

Sheikh Habibu Othman 'Mazinge' aliwata Waislamu kumuomba Mwenyezi Mungu adumishe amani na umoja miongoni mwa Wazanzibari.



Kaimu Mkurugenzi Idara ya Habari Maelezo, Omar Saidi, akimkabidhi cheti cha ustaafu aliyekuwa mfanyakazi wa Idara ya Habari Maelezo kitengo cha vipaza sauti, Omar Sleiman Othman, Mjini Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maalim ataka ufumbuzi soko lililosuswa na wavuvi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ameutaka uongozi wa Wilaya ya Micheweni Kisiwani Pemba kukutana na wadau wa soko la Wingwi Njuguni kumaliza mvutano uliopo baina ya uongozi wa halmashauri na wauza samaki wa sokoni hapo, ambao wamelisusia.

Alisema ni vyema wana siasa, halmashauri na wauza samaki kukaa pamoja ili kutafuta njia bora kuliendeleza soko hilo ambalo lilizinduliwa mwaka jana.

Maalim Seif aliyaeleza hayo alipofanya ziara ya kushtukiza katika soko hilo juzi jioni kulikagua kwani tangu kujengwa kwa soko hilo, wavuvi waligoma kuingia na kuendelea na kazi zao katika eneo lao la zamani kwa madai kuwa limejengwa mbali na barabara na halina wateja ikilinganishwa na eneo walilo sasa.

Maalim Seif alisema mara nyingi watu wanapoambiwa wahamie eneo jipya wanajisikia uzito kutokana na hilo aliutaka uongozi wa wilaya kuondoa changamoto ziliopo ili wauza samaki waweze kuingia sokoni.

"Ni vyema tukakaa pamoja kujadiliana ili tuone njia sahihi za kuchukuwa ambazo zitaleta faida kwa wadau wote wa soko hili alisema," alisema Maalim Seif.

Wauza samaki wa soko hilo walisema kawaida huwauzia samaki wapita njia lakini kutokana na soko hilo kujengwa mbali na barabara wateja wao hawawezi kuingia hivyo ni changamoto kibiashara.

"Tuliingia katika soko hili lakini kutokana mahali liliko wote tulikata misingi, (mitaji) kwa sababu wateja hawaji kununua sisi tukaona turudi eneo letu la zamani," alisema Issa Hassani ambaye ni muuza samaki wa eneo hilo.

Hassan alisema waliona bora walipe kodi kubwa, lakini wako katika eneo ambalo wateja wao wanaliona na biashara zinafanyika ili kupata fedha za kujikimu.

Akizungumza mbele ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Mbwana Hamad Shehe, alisema walifanya miundombinu bora katika soko hilo lakini wavuvi walikataa kuingia sokoni hapo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## KUPOTELEWA NA CHETI



DEUS MADALALI ANATANGAZA KUPOTELEWANA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S.1777-0012 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA NYAMALIMBE SEKONDARI MWAKA 2014.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/872264/2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

NERBAT J. MWASIKA anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC 213 CCT - TVS KING. Chassis No. MD6M14PA9J4N84311. Engine No. AK4NJ4101043. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: SON/TUN/RB/885358/2020

## ANATAFUTWA DEREVA

Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784 691605 / 0715 691605.

## JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

Katika mahakama ya mwanzo **MAKOLE**
Usimamizi wa mirathi **2021**
Ombi la **SADALLAH IBRAHIM SADALLAH** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu **KHAMIS SHABANI MALONGO**
KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO.
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe **18/01/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Tarehe **4/01/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HASMA SELENDA MSANGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SPACIO** yenye namba za usajili **T 208 BEH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/RB/4637/2018.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 203 YA 2020**
**BAINA YA**
**MESHACK CHIWANGA.................................... MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DAVID MGONGO NA WENZAKE ......................... WADAIWA**

**KWA: -**
**DAVID MGONGO**
**JANE WILSON**
**FAUSTIN MASSI**
**OSWARD**
**AMONI**
**ARON GABNUS**
**HAIBA A. MATUS**
**BAHATI E. FUIME**
**KEVIN A. LIKUNI**
**TARRAN WAZIR**
**EMMY MBONDE**
**THOMAS T. AIKARUWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.

**Kwa hiyo** unatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binafsi,wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tareh 5/1/2021 saa 3;00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta uetetzi weko kwa maandishi.

**Angalizo:** - kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 4ya mwezi wa Januari,2021.

..............................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 203 YA 2020**
**BAINA YA**
**MESHACK CHIWANGA....................................... MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DAVID MGONGO NA WENZAKE ..............WADAIWA**

**KWA: -**
**KHALIFA NJOU**
**PENDO**
**MIRIAM MCHAWI**
**HASSAN NDUNYI**
**ABRAHAM A. ALLY**
**AGATHA F.**
**RICHARD LENGAI**
**RUTH MDEE**
**GODFREY**
**ISMAIL**
**JUMANNE CHARLES**
**LUCY**
**POPOTE WALIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.

**Kwa hiyo** unatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binafsi,wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tareh 5/1/2021 saa 3;00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta uetetzi weko kwa maandishi.

**Angalizo:** - kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 4ya mwezi wa Januari,2021.

..............................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 203 YA 2020**
**BAINA YA**
**SIMON CHIWANGA....................................... MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PACAL M. KAGUSA NA WENZAKE ..............WADAIWA**

**KWA: -**

| | |
|---|---|
| **PASCAL M. KAGUSA** | **HOSEA MWANTEU** |
| **ALLY A. SACOKA** | **DEO MBOYA** |
| **EMMY MBONDE** | **ISMAIL** |
| **DAVID MSAHALA MABWAI** | **DANIEL MWANI TEVU** |
| **RABIA ALLY** | **MATHA JOHN RAJAB** |
| **AGUSTINO** | **STEPHANO MICHAEL** |
| **KARIA MATHIA** | **ANTONY CLAUDI MDOMA** |
| **JACOB ELIZABETH** | **SIMONI MATUMBI** |
| **GRADINO COSMAS** | **GIDION STEPHANO TOGWA** |

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.

**Kwa hiyo** unatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binafsi,wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tareh 5/1/2021 saa 3:00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta uetetzi weko kwa maandishi.

Angalizo: - kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 4 ya mwezi wa Januari,2021.

..............................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 203 YA 2020**
**BAINA YA**
**SIMON CHIWANGA....................................... MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PACAL M. KAGUSA NA WENZAKE ..............WADAIWA**

**KWA: -**

| | |
|---|---|
| **PATRIC WOISO** | **ASHA** |
| **MRISHO MALIKO MRISHO** | **JACOB ELIZABETH** |
| **SHIDA MARIO MWITA** | **KATARINA MATHI** |
| **AMOS ZEBEDAYO NOAH** | **MOHAMED WILLIUM** |
| **MLEWA** | **M.SAID** |
| **CARLOS** | **MRISHO** |
| **JULIUS** | **IDDI MARIA** |
| **SHAYO** | **MOHAMED HATH** |
| **PIUS** | **DEO MBOYA** |
| | **SEVERIN MZORA** |

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**Kwa kuwa** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.

**Kwa hiyo** unatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binafsi,wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tareh 5/1/2021 saa 3:00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta uetetzi weko kwa maandishi.

**Angalizo: -** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 4 ya mwezi wa **Januari, 2021.**

..............................................
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

## OFISI ZA MATANGAZO
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanafunzi Kenya warudi shuleni baada ya miezi tisa

**Nairobi, KENYA**

SHULE zote nchini Kenya, zimefunguliwa baada ya serikali kuzifunga tangu mwaka jana, kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Baada ya miezi tisa ya shule zote kufungwa kwa sababu ya COVID-19, hatimaye wanafunzi milioni 16 wanatarajia kurejea shuleni.

Kufungwa kwa shule nchini Kenya, Machi mwaka jana, kuliathiri watoto, huku idadi kubwa wakitarajiwa kuacha shule baada ya kusalia nyumbani kwa muda mrefu, licha ya baadhi ya shule kuweka utaratibu wa wanafunzi kusoma kwa njia ya intaneti.

Hata hivyo, Wakenya wachache walipata vifaa muhimu vya kiteknolojia ili kusoma kwa njia hiyo.

Kulingana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), wasichana zaidi ya wawili kati ya watano, hivi sasa wana ujauzito nchini Kenya.

Aidha, wasichana walioachwa na wazazi wao waliendelea kufanya kazi na wengine waliolewa.

Serikali imeahidi kutoa barakoa kwa wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuzinunua kama anavyofafanua Dk. George Magoha, ambaye ni waziri wa elimu.

"Serikali itatoa madawati 500,000 kwa shule, kuhusu suala la barakoa, hatuna mjadala, kwa kuwa wanafunzi wote watakaoingia shuleni watapewa."

Pia, shule zimetakiwa kuhakikisha kuwa zina vifaa vya kutosha vya kukabiliana na janga la corona kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya.

Upande wa michezo shuleni kama vile uigizaji, muziki, kandanda na hafla za kuwatuza wanafunzi zawadi, vimepigwa marufuku kwa kipindi cha siku 90.

Dk. Magoha alisema ana imani kuwa wanafunzi watafidiwa muda waliopoteza shule zilipokuwa zimefungwa.

Kufunguliwa kwa shule mwezi huu nchini Kenya, kunatarajiwa kukamilisha muhula wake katikati ya mwezi Machi, mwaka huu.

***RFI/DW***



Wanafunzi wakiwa darasani. Mamilioni ya watoto wanaosoma shule za msingi na sekondari nchini Kenya, wamerejea shuleni, huku kukiwa na masharti kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA/REUTERS**

# Waliouawa kwa shambulizi Niger wafikia watu 100

**Niamey, NIGER**

WAZIRI Mkuu wa Niger, Brigi Rafini, amesema watu 100 wameuawa kwenye shambulizi mwishoni mwa wiki, yaliyotekelezwa na watu wanaoshukiwa kuwa wapiganaji wa Wajihad katika vijiji viwili.

Alisema watu 70 waliuawa katika kijiji cha Tchombangou, huku wengine 30 wakiuawa katika kijiji cha Zaroumdareye, mpakani mwa Niger na Mali.

Shambulizi hilo linatajwa kuwa baya zaidi kutokea, wakati nchi hiyo ikiendelea kupambana na vita vya kikabila na wanamgambo wa Kiislamu.

Hakuna kundi ambalo limedai kuhusika na mauaji hayo.

Kulingana na meya wa eneo la vijiji hivyo, Almou Hassane, waliohusika walisafiri kwa kutumia pikipiki 100, Shirika la Habari la AFP, lilisema.

Inasemekana wanamgambo hao waligawanyika katika makundi mawili na kutekeleza mashambulizi hayo kwa wakati mmoja.

Issoufou Issaka, ameiambia AFP kwamba, wapiganaji wa jihad walitekeleza mashambulizi hayo, baada ya wanavijiji kuwaua wanachama wao wawili, ingawa haijathibitishwa rasmi.

Meya Hassane, alisema baada ya mashambulizi hayo wanavijiji 75, waliachwa wakiwa na majeraha huku wengine wakipelekwa kupata matibabu katika eneo la Ouallam, mji mkuu wa Niamey.

Waziri Mkuu Rafini alitembelea vijiji hivyo Jumapili.

"Hali ni mbaya... lakini uchunguzi utafanywa ili waliohusika waweze kukabilika kisheria," aliwaambia wanahabari.

Eneo la Tillabéri huko Niger, lipo mpaka wa pande tatu Niger, Mali na Burkina Faso, kwa miaka mingi kumekuwa na mashambulizi ya wanamgambo wa jihad.

Mashambulizi ya hivi karibuni, yametokea eneo la Tillabéri na yamefanyika wakati nchi ya Niger, inaendeleza uchaguzi baada ya Rais Mahamadou Issoufou, kujiuzulu, aliyekaa madarakani kwa mihula miwili ya miaka mitano.

Aidha, maofisa wa uchaguzi wametangaza matokeo ya awali, Mohamed Bazoum, aliyekuwa waziri na mwanachama wa chama tawala cha Niger, ameashiria kuibuka na ushindi.

***BBC***

# 2020 K. Kusini ilishuhudia idadi kubwa ya vifo kuliko vizazi

**Seoul, KOREA KUSINI**

KWA mara ya kwanza Korea Kusini imerekodi vifo vingi kuliko vizazi mwaka jana, huku tahadhari ikitolewa katika nchi hiyo ambayo ina kiwango cha chini cha watu kuzaliwa.

Watoto 275,800 pekee walizaliwa mwaka jana, ikiwa ni chini ya asilimia 10 kutoka 2019 huku watu 307,764 wakifariki.

Takwimu hizo zimesababisha Wizara ya Mambo ya Ndani, kutaka mabadiliko ya kimsingi kwenye sera zake na kwamba idadi ya watu kupungua ni tatizo katika nchi.

Inaelezwa, mbali na kuwapo matumizi makubwa ya umma hasa mahitaji ya huduma za afya, pensheni, kupungua kwa idadi ya vijana pia kutasababisha uhaba wa nguvukazi ambayo inaathari moja kwa moja uchumi.

Desemba, mwaka jana, Rais Moon Jae-in alizindua mipango na sera kadhaa zinazolenga kushughulikia tatizo hilo, ikiwamo kukabiliana na tatizo la idadi ndogo ya vizazi, ikiwamo kutoa cha motisha ya pesa kwa familia.

Katika mpango huo, kuanzia mwaka 2022, kila mtoto aliyezaliwa atapata bonasi Dola 1,850 (Sh. milioni 4.2), kusaidia kulipia gharama kabla kuzaliwa, malipo ya kila mwezi hadi mtoto atakapofikisha umri wa mwaka moja. Pia, motisha kila mwezi itaongezwa hadi ifikapo 2025.

Inaelezwa, wanawake Korea Kusini, wanajitahidi kufikia usawa kati wa kufanya kazi na mahitaji mengine ya maisha, kwamba kuimarisha kipaji au kazi ni kipaumbele kuliko masuala ya uzazi.

***BBC***

## 'Democratic' kuliongoza Baraza la Wawakilishi

**Washington, MAREKANI**

NANCY Pelosi, amechaguliwa tena kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi la Marekani, kipindi cha nne, akiwa na wawakilishi wachache wa Chama cha Democrat.

Pelosi ambaye anatoka Jimbo la California, alipata kura za ushindi zilizopigwa juzi, alasiri, huku Wademocrat wawili wakipigia kura wagombea wengine na watatu wakipiga kura ya bila kuunga mkono wala kukataa.

Katika Baraza la Wawakilishi Wademocrat ni 222 na Warepublican 211.

Wawakilishi wengine wachache hawakuweza kupiga kura kwa sababu walikuwa wameambukizwa virusi vya corona au walikuwa na shida zingine za kiafya.

Kwa mara ya kwanza tangu Mei, wabunge walipaswa kuwapo kwenye upigaji kura, badala ya kutumia mfumo wa mtandao uliowekwa kipindi cha corona.

Kura hiyo ilidumu kwa saa kadhaa wakati wabunge waliletwa ndani ya ukumbi katika vikundi vidogo vidogo ili kuepusha idadi kubwa ya wajumbe ukumbini.

Bunge jipya linatakiwa kufufua uchumi wa nchi na kulishinda janga la corona ambalo hadi sasa limegharimu maisha ya Wamarekani zaidi ya 350,000.

***VOA***

# ARTETA

## AMTAJA TIERNEY UNAHODHA ARSENAL



**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaamini, Kieran Tierney, anaweza kuwa nahodha wa Arsenal, wakati mlinzi huyo wa kushoto wa zamani wa Celtic akiwa kwenye kiwango bora zaidi kwa sasa.

Tierney amecheza katika mechi zote kasoro moja kati ya 17 za Arsenal za Ligi Kuu msimu huu na alifunga bao la kwanza la kuvutia wakati wakishinda 4-0 dhidi ya West Brom, Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alipanda na mpira kutoka winga ya kushoto na kumchenga Sam Johnstone akafunga bao la ufunguzi, kabla ya Alexandre Lacazette kufunga la pili dhidi ya kikosi hicho cha kocha Sam Allardyce.

Ulikuwa ni ushindi wa tatu mfululizo kwa Arsenal, ambao wamepindua kiwango chao kibovu cha kutopata ushindi kwenye mechi saba.

Tangu mwanzoni mwa Desemba, hakuna mlinzi kwenye ligi aliyetengeneza nafasi nyingi kuliko Tierney (15), wakati Andy Robertson (29), Aaron Cresswell (25), Trent Alexander-Arnold (23) na Joao Cancelo (22) ni mabeki pekee waliotengeneza nafasi zaidi ya Mscotland huyo wa Arsenal ambaye kwa jumla yake hadi sasa ametengeneza nafasi 21.

Tierney alipata uzoefu wa unahodha wakati wa siku zake za mwisho kule Celtic kabla ya kuhamia Arsenal mwaka 2019, na Arteta ameona ubora wa uongozi kwa mlinzi huyo.

"Nafikiri anaweza kuwa," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kama Tierney anaweza kuwa nahodha wa 'Washikabunduki' hao siku moja.

"Ananidhamu na heshima na timu yote ya uongozi pamoja na wachezaji wanavutiwa naye sana.

"Hivyo ndivyo alivyo. Ni kijana mwenye aibu, lakini nafikiri anawasilisha thamani yake yote."

# PIRLO AMTAKA GIROUD JUVENTUS

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo, amesema mshambuliaji wa Chelsea, Olivier Giroud, atakuwa msaada mkubwa zaidi kama akisajiliwa kwa miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Giroud mwenye umri wa miaka 34, kwa mara nyingi anahusishwa na mpango wa kuondoka Chelsea baada ya kuanza katika mechi sita tu kwenye mashindano yote msimu huu.

Juve na Inter Milan ni miongoni mwa klabu zinazohusishwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, ambaye amefunga mabao tisa kwa Chelsea msimu wa 2020-21.

Pirlo alithibitisha Juventus watatafuta mshambuliaji wa ziadi wakati wa dirisha hili dogo la usajili la Januari.

"Giroud? Tunaweza kumtumia," alisema akiiambia DAZN baada ya kushinda mabao 4-1 kwenye mchezo wa Serie A dhidi ya Udinese.

"Lakini mambo yote hayo anayajua zaidi (Mkurugenzi wa michezo Fabio) Paratici kuliko mimi.

"Tulizungumza kuhusu hilo, lakini ngoja tuone kama tutafanya kitu fulani ndani ya siku chache zijazo."

Juventus ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi, pointi 10 nyuma ya vinara AC Milan, ingawa wana mchezo mmoja mkononi.



# FIFA YASUBIRISHA ADHABU YA TRIPPIER

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), limesimamisha adhabu ya kufungiwa kwa wiki 10 kwa makosa ya kubashiri yanayomkabili, Kieran Trippier, baada ya Atletico Madrid kukata rufani.

Mlinzi huyo alifungiwa na kutozwa faini ya pauni 70,000 Desemba 23, mwaka jana baada ya Chama cha Soka cha England (FA), kumkuta na hatia kwa kukiuka kanuni ya sheria E8 (1) (b).

Kanuni hiyo inasema: "Pale mshiriki anapompa mtu mwingine yeyote habari yoyote inayohusiana na mpira wa miguu, ambayo mshiriki amepata kutokana na msimamo wake ndani ya mchezo na ambayo haipatikani hadharani wakati huo, mshiriki atakuwa amekiuka sheria hii, ambapo habari yoyote hiyo inatumiwa na mtu huyo mwingine, kuhusiana na kubashiri. "

Trippier, ambaye alikanusha mashtaka hayo, alikuwa akikabiliwa na uwezekano wa kukosa kucheza michezo 14 ya Atletico hadi Februari 28, ambayo inajumuisha mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea.

Lakini, mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 30, atakuwa huru kucheza tena wakati mchakato wa kukata rufani ukiendelea.

Msemaji wa FIFA alithibitisha Jumapili: "Kufuatia rufani na, haswa, ombi la hatua za muda zilizowasilishwa na klabu ya Atletico Madrid, Kamati ya Rufani ya FIFA imeidhinisha kusitisha muda wa kusimamishwa dhidi ya Kieran Trippier hadi hapo utaratibu utakapomalizika. "

Trippier alikosa mchezo wa Jumapili wa ushindi wa Atletico dhidi ya Deportivo Alaves baada ya kuachwa kikosini.

## HABARI MICHEZO



# MESSI
## AFIKISHA MECHI 500 LALIGA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi alicheza mechi yake ya 500 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa Barcelona, Jumapili wakati walipocheza na Huesca.

Messia alirudi kwenye kikosi cha kocha Ronald Koeman baada ya kuwa nje ya dimba kutokana na kusumbuliwa na maumivu ya kifundo cha mguu na waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Messi aliukosa mchezo wa Jumanne wa sare ya 1-1 dhidi ya Eibar baada ya kupewa mapumziko ya Sikukuu ya Krismasi.

Hata hivyo, Koeman aliamua kumrudisha kikosini nahodha huyo mwenye umri wa miaka 33 na akaweka historia ya kucheza mechi 500.

Rekodi ya Messi ya kucheza mechi 500 kwenye Ligi Kuu kwa Barca imemfanya kubakiwa na mechi tano tu kuifikia rekodi iliyowekwa na Xavi.

Xavi pia ndio anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi kwa 'Blaugrana' hao katika mashindano yote akicheza mara 767.

Kwa ujumla Xavi amecheza mechi 17 zaidi ya Messi ambaye kwa sasa ana mechi 750 katika mashindano yote kwa Barcelona.

## GUARDIOLA: CITY IMERUDI KWENYE UBORA WAKE

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anahisi Manchester City imerudi kwenye kiwango chake ambacho kiliwawezesha kushinda taji la Ligi Kuu England mara mbili mfululizo, baada ya kuwafunga Chelsea, juzi Jumapili.

Licha ya kuwa bila nyota wake sita kwenye kikosi cha kwanza kutokana na virusi vya corona, City waliwafumua Chelsea mabao 3-1 pale kwenye dimba la Stamford Bridge na hivyo kuwafanya kupata ushindi wa tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu.

Mabao yote yalifungwa kipindi cha kwanza, huku Kevin de Bruyne akitoa pasi ya mwisho kwa Phil Foden na baadaye akafunga mwenyewe baada ya kufunga la ufunguzi.

Baada ya kuwa na msimu mbaya wa 2019-20 na kuanza polepole msimu huu, Guardiola sasa anaona ishara nzuri kwa City baada ya mchezo dhidi ya Chelsea.

"Ni timu ileile. Kocha yuleyule, na benchi la ufundi ni lilelile," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports mara baada ya mchezo huo.

"Kocha msaidizi alibadilika. Lakini wachezaji ni wale wale na hamasa ni ile ile.

"Namna walivyoshinda mataji ya ligi ndivyo walivyocheza leo. Hamasa haikuwapo, lakini sasa imerudi na tumeimarika vizuri sana."

Tangu walipopoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Tottenham, Novemba, City imeshinda mechi tano kati ya saba za Ligi Kuu na kutoka sare mbili.



## LAMPARD ATAKA UVUMILIVU CHELSEA

**LONDON, England**

FRANK Lampard amekubali kwamba, Chelsea "walipata somo zuri" kutoka kwa Manchester City kwa kipigo cha Jumapili, lakini amesisitiza watu wanatakiwa kuwa wavumilivu.

Kikosi cha Pep Guardiola kiliibuka na ushindi wa mabao 3-1 pale Stamford Bridge, huku Ilkay Gundogan, Phil Foden na Kevin De Bruyne wote wakifunga kipindi cha kwanza.

Chelsea, walifunga bao la kufutia machozi kupitia kwa Callum Hudson-Odoi dakika za majeruhi, ambapo walifanikiwa kupiga mashuti mara mbili tu langoni.

Blues hao sasa wamepoteza mechi nne kati ya sita za ligi.

Wamepata pointi 26 kutoka mechi 17 za ligi msimu huu wa 2020-21, tatu chache zaidi kama walizozipata kipindi kama hiki msimu uliopita, na hawajawahi kumaliza zaidi ya nafasi ya sita juu baada ya kushindwa kufikisha pointi zaidi ya 26 kwa wakati kama huu kwenye msimu.

Huku Liverpool na Manchester United wakiwa kileleni mwa msimamo wakiwapita pointi saba na mchezo mmoja mkono, presha imekuwa kubwa zaidi kwa Lampard, ambaye alitumia kiasi cha pauni milioni 220 kwenye usajili uliopita.

Na sasa Lampard anataka uvumilivu zaidi wakati kikosi chake kikizidi kuimarika zaidi.

"Kwa dakika 10 za mwanzo tulikuwa vizuri, halafu tukaanza kuruhusu mabao mawili kwa hakika yalikuwa mabao ya kipuuzi.

"Lakini kwa sasa tunahitaji uvumilivu kwa kiasi kikubwa zaidi," alisema Lampard.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KOEMAN AMCHOKA GRIEZMANN BARCA

●●●Tumekosa nafasi tisa za kufunga kwenye mchezo mmoja, lakini haimaanishi chochote hasa kwa kumtoa Antoine...

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amesema Barcelona walikosa nafasi tisa za kufunga wakati walipopata bao moja katika mashuti 20 na kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Huesca, na ameitaka klabu hiyo kusajili straika mpya.

Lionel Messi alirudi kwenye kikosi cha Barcelona baada ya kupona kifundo cha mguu na Koeman aliamua kumchezesha nafasi ya mshambuliaji wa kati pamoja na Martin Braithwaite na Ousmane Dembele.

Watatu hao walijaribu kufunga kwa mashuti 15, lakini alikuwa ni Frenkie de Jong ndiye aliyefunga bao hilo pekee, akiunganisha pasi ya Messi katika dakika ya 27.

Koeman, ambaye alimwingiza Antoine Griezmann kuchukua nafasi ya Braithwaite dakika tisa kabla ya mchezo kumalizika, alikubali kwamba anahitaji kutafuta mshambuliaji ili kuongoza safu ya mashambulizi kwa kusaidiwa na Messi na Dembele.

"Namwamini kila mchezaji kwenye kikosi chetu," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Jumapili usiku.

"Lakini kama ukichagua viungo watatu kuna nafasi ya washambuliaji watatu mbele.

"Kwa uwapo wa leo na pembeni akiwa Dembele, na hivyo tunatakiwa kuchagua kati ya Martin au Antoine mbele na Martin amefanya hivyo mara nyingi.

"Tumekosa nafasi tisa za kufunga kwenye mchezo mmoja, lakini haimaanishi chochote hasa kwa kumtoa Antoine.

"Tuna michezo mingi mbele yetu na tunawahitaji wachezaji wote hao.

"Tumesema mara kadhaa, mwanzoni mwa msimu, kwamba tunataka mtu mbele ambaye ana uwezo wa kushindana kufunga mabao zaidi, lakini hilo linategemea na vitu vingi."

Koeman amesema anaamini wakiimarisha safu yao ya ushambuliaji, itapunguza presha kwenye safu yao ya ulinzi.

Barcelona mashuti yaliyolenga bao ni saba tu kati ya 20 na Koeman amesema wanatakiwa kumaliza mchezo mapema.

"Kipindi cha pili kilikuwa bora zaidi kwa upande wetu," alibainisha Koeman.

## KWA UFUPI

**SPURS WATETA NA KANE**

TOTTENHAM Hotspur imeanza majadiliano na straika, Harry Kane kuhusu kumwongeza mkataba. Nahodha huyo wa England mwenye umri wa miaka 27, alisaini mkataba wa miaka sita mwaka 2018, na Mwenyekiti Daniel Levy anataka kuzima ndoto za Manchester City na Paris St-Germain wanaomwania. ***(Independent)***

**LAMAPRD HALI TETE**

KAZI ya Frank Lampard kama kocha wa Chelsea ipo kwenye tishio kubwa na klabu imeaanza kuangalia mipango mbadala. (The Athletic)

**TORREIRA KURUDISHWA ARSENAL**

ARSENAL ipo tayari kumrudisha kiungo wa Uruguay, Lucas Torreira kutoka Atletico Madrid anakocheza kwa mkopo, huku Fiorentina ikionyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(La Nazione via Express)***

**PSG WAMTAKA KEAN JUMLA**

KLABU ya Paris St-Germain ipo kwenye mazungumzo ya makubaliano na mshambuliaji wa Everton, Moise Kean mwenye umri wa miaka 20 raia wa Italia, ili kumpa mkataba wa kudumu kutoka ule wa mkopo wa muda mrefu, wenye thamani ya pauni milioni 31. ***(Sky Sports)***

**POCHETTINO KUIFUMUA PSG**

KOCHA mpya wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino ataruhusiwa kukifanyia mabadiliko kikosi - na hiyo inamaana kwamba, kunaweza kuwa na usajili wa haraka wa kiungo wa Tottenham, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24**. *(Mirror)***

**JUVE KUMUUZA DYBALA**

STRAIKA wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham na Manchester United, atauzwa na Juventus kipindi kijacho cha majira ya joto, kama hatasaini mkataba mpya. ***(Tuttosport via Football Italia)***

**SOLSKJAER KUWATOA SITA**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, atafanya mazungumzo na wachezaji wake wakati huu wa dirisha dogo la usajili la Januari kuhusu mipango yake, na wachezaji sita wanaweza kutolewa kwa mkopo au kuuzwa moja kwa moja. ***(Sun)***

**DIALLO KUTOBAKI ATALANTA**

MANCHESTER United itakataa ombi la Atalanta la kutaka kumbakiza winga wake raia wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 18, ambaye anacheza kwa mkopo kwa miamba hao wa Serie A na wanataka kubakia naye hadi mwishoni mwa msimu. ***(ESPN)***

**LACAZETTE KUJADILIWA ARSENAL**

KOCHA Mikel Arteta amesema Arsenal watajadili majaliwa ya straika wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29 kipindi cha majira ya joto. ***(Standard)***

**DIGNE MKATABA MPYA EVERTON**

MLINZI wa Ufaransa, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kusaini mkataba mpya na Everton. ***(Liverpool Echo)***

**JORDAN ANA FURAHA SEVILLA**

KIUNGO wa kimataifa wa Hispania, Joan Jordan mwenye umri wa miaka 26, amesema anafuraha pale Sevilla, huku akihusishwa na Arsenal. ***(Football London)***

HABARI MICHEZO

## NIC yatoa mamilioni Kombe la Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI mashindano ya Kombe la Mapinduzi yakianza leo, Shirika la Bima la Taifa (NIC), limeingia 'mazima' kudhamini michuano hiyo kwa kutoa zawadi maalumu kwa mchezaji bora wa kila mechi, limeeleza.

Mkurugenzi Mkuu wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, ndiye aliyetangaza udhamini huo wakati akizungumza na Kamati ya Kombe la Mapinduzi pamoja na uongozi wa Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo kwenye mkutano uliofanyika Migombani katika ofisi za wizara hiyo jana.

Alisema mbali ya udhamini wa mchezaji bora wa kila mchezo, lakini watachangia msaada maalum katika uendeshaji wa mashindano hayo kwa kuwa lengo lao kuu ni kudumisha umoja uliopo kati ya Zanzibar na shirika hilo, pamoja na kuunga mkono Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, ambayo yanatimiza miaka 57 sasa.

"Kwa awamu hii tumetenga Sh. milioni 14.7 kwa ajili ya udhamini wa mashindano hayo, ambazo zitakuwa kwa ajili ya mchezaji bora kuanzia mechi ya kwanza hadi ya mwisho, pamoja na uendeshaji wa mashindano hayo," alisema.

Alisema kutokana na mashindano hayo kuvuta hisia kwa wananchi wengi kutokana na umuhimu wake, shirika hilo limejitolea kutoa udhamini kama huo kwa kipindi cha miaka mitatu, kuanzia 2021 hadi 2023.

## Ligi Z'bar zapisha Mapinduzi Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Kuu Zanzibar, imesimamisha ligi hiyo pamoja na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, ili kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo inaanza kutimua vumbi visiwani hapa leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa bodi hiyo, Sheha Mohmmed Ali, alisema ligi hizo mbili zinasimama wakati Ligi Kuu Zanzibar kila timu ikiwa imeshacheza michezo minane huku Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kila timu ikicheza mechi tatu.

Alisema kusimama kwa ligi hiyo ni kawaida kila mwaka kwa kipindi kama hiki kutokana na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kuwa katika jukumu lingine la kusimamia michuano hiyo.

Alisema bodi ya Ligi Kuu baadaye itakutana na klabu zote, ili kupanga tarehe ya kuendelea kwa ligi pamoja nakujadili kufungua dirisha dogo la usajili katika kipindi hiki ambacho michuano ya Kombe la Mapinduzi ikiendelea.

"Ligi zimesimama ili kupisha Kombe la Mapinduzi, hivyo timu ambazo zimepata fursa ya kushiriki mashindano hayo zitashirki michuano hiyo, na zile ambazo hazijapata fursa ya kushiriki basi zitatumia muda huu wa kusimama kwa ligi kujiandaa na kuendelea na ligi hapo itakaporejea," alisema.

# SIMBA: MKUDE HAJAFUKUZWA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wakijiandaa kushuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kuikaribisha FC Platinum ya Zimbabwe, uongozi wa mabingwa hao wa Tanzania Bara, umesema kiungo Jonas Mkude, hajafukuzwa ndani ya kikosi hicho.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo Desemba 28, mwaka jana ilieleza kuwa, imemsimamisha Mkude ndani ya kikosi hicho kutokana na tuhuma za utovu wa nidhamu hadi hapo Kamati ya Nidhamu ya Simba itakapotoa uamuzi.

Lakini akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana kuelekea mechi yao dhidi ya FC Platinum, Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara, alisema suala la Mkude bado lipo mikononi mwa Kamati ya Nidhamu ya klabu hiyo na mchezaji huyo hajafukuzwa.

**"Ijulikane tu kuwa mpaka sasa Jonas Mkude ni sehemu ya Simba, hajafukuzwa kazi, amepitia changamoto kama mfanyakazi mwingine kokote.**

"Mkude ni mchezaji wa Simba. Jambo lake lipo kamati ya maadili, hajafukuzwa. Bila shaka yoyote baada ya kamati atarejea klabuni. Huyu ndiye mchezaji mwandamizi ndani ya Simba kwa miaka 10," alisema.

Tayari Mkude amekosa mechi mbili, ya kwanza ikiwa Kombe la Shirikisho dhidi ya Majimaji na ya pili ni ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC zote zilichezwa Uwanja wa Mkapa na Simba kushinda 5-0 na 4-0.

Katika mechi ya kesho, Simba inakabiliwa na kibarua kigumu cha kupindua matokeo ikitakiwa kushinda kuanzia mabao 2-0 ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo kutokana na wapinzani wao kuwa mbele kwa bao 1-0, ushindi walioupata kwenye mechi ya awali mjini Harare, Zimbabwe wiki mbili zilizopita.

ACHENI WAJE...



Wachezaji wa Taifa Stars, wakiwa mazoezini katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana, wakati huu timu hiyo ikijiandaa na mechi mbili za kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zitakazopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Januari 10 na 13, kama sehemu ya maandalizi ya fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) zitakazofanyika nchini Cameroon kuanzia Januari 16 hadi Februari 7, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mastraika Tanzania tatizo - Kocha Mbeya

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema kuna tatizo la ufungaji kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hasa kwa wachezaji wa Kitanzania, hivyo kufanya kusiwe na idadi kubwa ya mabao katika ligi hiyo pendwa ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Akizungumzia tathmini ya timu yake ya Mbeya City ambayo haifanyi vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Lule ambaye ni raia wa Uganda, amesema hata kwenye timu yake nafasi wanapata, lakini tatizo ni kutumbukiza mpira ndani ya nyavu.

"Halafu hili tatizo naona ni tatizo la wachezaji wengi wa Tanzania, ndiyo maana utaona hata matokeo ya mechi nyingi yanakuwa ni bila kufungana, bao 1-1, 1-0 au 2-1, ni mara chache kuona timu inafungwa zaidi ya mabao hayo, halafu ni kwa timu ambazo zina wachezaji wengi ambao mastraika wao ni wa kutoka nje ya nchi," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema tatizo hilo analifanyia kazi angalau lipate kurekebishika kwenye timu yake, ingawa si kwa kulitatua kabisa kwa msimu huu.

Mbeya City ilitoka suluhu dhidi ya KMC Jumapili kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kuzifanya timu hizo kugawana pointi moja moja.


Kwa sasa Mbeya City iko kwenye nafasi ya 17, moja juu ya ndugu zao Ihefu FC ambao nao ni wa Mbeya, wakati huu wakiburuza mkia wakiwa na ponti 13.

Mbeya City ina pointi moja zaidi ya Ihefu, ikicheza mechi 18, kushinda mechi mbili, sare nane na kupoteza mechi nane pia.

# Michezo

Jumanne Januari 5, 2021

Nipashe

## KOEMAN AMCHOKA GRIEZMANN BARCA

HABARI UK 22



HAWATOKI...

Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mchezo wao wa kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho saa 11 jioni. Kushoto ni Meneja Masoko wa Simba, George Abdlrahman. PICHA: JUMANNE JUMA

# SIMBA: FC PLATINUM MBONA MAPEMA TU

●●●CAF yabadili muda, Wazimbabwe nao wasema watawatoa kama UD Songo ilivyowatoa, Mkude atajwa...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Simba tayari umeshinda vita ya kwanza ya ombi la mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum kuchezwa Jumatano saa 11:00 jioni badala ya saa 1:00 usiku na kutokana na hatua hiyo, umesema mapema tu kabla ya jua kuzama lengo lao la kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo litatimia kesho.

Simba iliandika barua Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kuomba kuongezewa idadi ya mashabiki kuingia uwanjani kwa asilimia 100 katika mechi ya marudiano dhidi ya FC Platium ya Zimbabwe ikiwa ni pamoja na mechi hiyo ya kesho kuanza saa 11:00 jioni badala ya saa 1:00 usiku.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema tayari ombili hilo la kurudishwa nyuma muda wa mechi limekubaliwa na wanachosikilizia ni ruksa ya kuingiza mashabiki kwa asilimia 100.

“Tumeruhusiwa kucheza saa 11:00 jioni, tunasubiri majibu ya ombi letu kuhusu kuruhusiwa kujaza uwanja kuingiza mashabiki kwa asilimia 100, kwa sababu kwetu hali ni nzuri, hatuna ugonjwa wa Covid-19.

“Tumeruhusiwa mashabiki kuingia kwa asilimia 50, hivyo kwa sasa tutauza tiketi kulingana na maelekezo ya awali ambayo tulipewa na CAF, endapo tutaruhusiwa kuongeza idadi ya mashabiki tutaendelea kuuza tiketi zingine,” alisema Manara.

Manara aliongeza: “Tunaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kuja kutoa sapoti kwa timu yetu, ninaamini wakija kwa wingi huku wakiimba ‘WIDA, WIDA, WIDA...’ kwa wingi wetu FC Platinum hawatoki, kwa sababu tumejipanga vizuri kupata ushindi katika mechi yetu hiyo.”

Alisema licha ya kuwapo kwa baadhi ya mashabiki wa timu pinzani nchini kuiombea Simba itolewe na Wazimbabwe hao, ana uhakika mapema tu kabla ya saa 1:00 usiku timu hiyo itakuwa imeitoa FC Platinum na kutinga hatua ya makundi.

“Kama wapinzani wetu (wa ndani) wanataka kupanda ndege msimu ujao, basi waiombee Simba iitoe Platinum maana tukisonga mbele kuna nafasi ya kusaidia kuingiza timu nne msimu ujao, vinginevyo wataendelea kupanda Saibaba na mabasi mengine maana Simba itaendelea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na kushiriki michuano hiyo,” alisema.

Kuhusu viingilio vya mechi hiyo, Manara alitangaza kuwa kwa VIP A ni Sh. 40,000, Platinum Sh. 150,000, VIP B na C ni Sh. 30,000 huku mzunguko akisema ni Sh. 7,000 tu.

Na kwa upande wa suala la Kiungo Jonas Mkude, Manara alisema bado linashughulikiwa na Kamati ya Nidhamu ya Simba na baada ya kujiridhisha, nyota huyo atarejea kikosini.

“Mkude ni miongoni mwa wachezaji wa Simba tena msimu huu anatimiza miaka 10 akitumikia klabu hii bila kuondoka, hivyo suala lake lipo katika utaratibu na kamati inafanya kazi yake,” alisema Manara.

Lakini kwa upande wa Kocha wa FC Platinum, Norman Mapeza, amesema hakuna kisichowezekana na wamekuja Tanzania kufanya kama UD Songo ya Msumbiji msimu uliopita ambayo ilitoka sare tasa na Simba mjini Maputo na mechi ya marudiano katika Uwanja wa Taifa (kwa sasa Benjamin Mkapa) jijini Dar es Salaam, ikawatoa ‘Wekundu wa Msimbazi’ hao kwa faida ya bao la ugenini baada ya sare ya 1-1.

“Barcelona inafungwa, Manchester City inafungwa pia, timu zote kubwa zinafungwa hata Simba inaweza kufungwa nyumbani hakuna kinachoshindikana katika soka, kama UD Songo iliweza kwa nini sisi tushindwe,” alisema kocha huyo ambaye timu yake iliibuka na ushindi wa bao 1-0 nyumbani katika mechi ya kwanza.

# YANGA NA MAJEMBE 20 MAPINDUZI CUP LEO

**Hawa Abdallah, ZANZIBAR na Adam Fungamwango**

WAKATI mashindano ya 15 ya Kombe la Mapinduzi yakitarajiwa kuanza rasmi leo kati ya mabingwa watetezi, Mtibwa Sugar dhidi ya Chipukizi katika Uwanja wa Amaan saa 10:00 alasiri, vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga ambao watashuka dimbani hapo saa 2:15 usiku leo dhidi ya Jamhuri ya Pemba, tayari wametua visiwani hapa wakiwa na wachezaji 20.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Katibu wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi, Aiman Othman Douwe, alisema maandalizi yote ya yamekamilika kuelekea mashindano hayo ikiwamo timu za kutoka Pemba tayari zimewasili Unguja.

Alisema Kamati ya Kombe la Mapinduzi imefanya marekebisho ya ratiba kwa upande wa mchezo wa Simba badala ya kucheza Januari 7, sasa utachezwa Januari 8, mwaka huu majira ya saa kumi jioni, mabadiliko hayo ni kutokana na mchezo wao wa kimataifa dhidi ya FC Platinum utakaochezwa kesho, hivyo siku hiyo Azam ndiyo itacheza dhidi ya Mlandege.

Kwa upande wa kikosi cha Yanga, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, aliliambia Nipashe kuwa, wamewasili visiwani hapa jana jioni wakiwa na wachezaji 20, kocha Cedrick Kaze, pamoja na baadhi ya viongozi.

“Baada ya mapumziko ya siku mbili, kikosi kilirejea kambini na tuimeingia Zanzibar kwenye Kombe la Mapinduzi na kumbukeni kuwa hatukupeleka kikosi cha pili, tumepeleka kikosi chote. Ikumbukwe kuwa kwenye kikosi cha Yanga tuna wachezaji 28, sasa katika hao tunakwenda na wachezaji 10, ila tu tutamkosa nahodha wetu Lamine Moro ambaye ameomba ruhusa kwenda kusalimia familia kwa sababu tangu mwaka jana hakwenda kutokana na matatizo ya mlipuko wa corona,” alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042